JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

# HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI DKT. MAHMOUD THABIT KOMBO (MB.), WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

MEI, 2026

DODOMA

**HOTUBA YA MHESHIMIWA *BALOZI* DKT. MAHMOUD THABIT KOMBO (MB.), WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

# YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ....................................................................1
2.0 MISINGI YA TANZANIA KATIKA UHUSIANO WA KIMATAIFA ....................................................................7
3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 .................................................................... 13
3.1 Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026....................................................................14
3.2 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Kuzingatia Vipaumbele ....................................................................16
4.0 MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA UTATUZI WAKE ..........91
4.1 Mafanikio ....................................................................91
4.2 Changamoto na Hatua za Utatuzi Wake......................93
5.0 SHUKRANI ....................................................................96
6.0 MAPENDEKEZO YA VIPAUMBELE NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ....................................................100
6.1 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ....................................................................100
6.2 Vipaumbele vya Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 .................................101
7.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 .............................................104
8.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA TAASISI ZILIZO CHINI YAWIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ....................................................................109
9.0 HITIMISHO ....................................................................111

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AfCFTA | African Continental Free Trade Area |
| AfDB | African Development Bank |
| AGRF | Agri-Food Systems Transformation |
| AI | Artificial Intelligence |
| AICC | Arusha International Conference Centre |
| ALHC | African Liberation Heritage Centre |
| APRM | African Peer Review Mechanism |
| ASBF | Africa Singapore Business Forum |
| AU | African Union |
| COP | Conference of the parties |
| CRDB<br>DDH | Cooperative Rural Development Bank<br>Diaspora Digital Hub |
| Dkt | Daktari |
| DRC | Democratic Republic of the Congo |
| DSA | Digital Substraction Angiography |
| EAC | East African Community |
| EACJ | East African Court of Justice |
| EACOP | East African Crude Oil Pipeline |
| EALA | East African Legislative Assembly |
| EDCF | Economic Development Cooperation Fund |
| EFD | Electronic Fiscal Device |
| ESDP | Economic and Social Development Programme |
| FMD | Foot and Mouth Disease |

| | |
|---|---|
| FOCAC | Forum on China-Africa Cooperation |
| GGHSP | Grant Assistance on Grassroots Human Security Projects |
| IAEA | International Atomic Energy Agency |
| ICGLR | International Conference on the Great Lakes Region |
| IFAD | International Fund for Agricultural Development |
| IGAD | Intergovernmental Authority on Development |
| IORA | Indian Ocean Rim Association |
| ISIS<br>IUCEA | Islamic State in Iraq and Syria<br>Inter-University Council for East Africa |
| JNICC | Julius Nyerere International Convention Centre |
| JPC | Joint Permanent Commission |
| JPCC | Joint Permanent Commission Cooperation |
| JPCDS | Joint Permanent Commission on Defence and Security |
| LLDC<br>GLMC | Landlocked Developing Countries<br>Global Labor Market Conference |
| Mb | Mbunge |
| MCC | Millennium Challenge Corporation |
| MoU | Memorandum of Understanding |
| MRCC | Maritime Rescue Coordination Centre |
| MTCP | Malaysian Technical Cooperation Programme |
| MSD | Medical Stores Department |
| NATO | North Atlantic Treaty Organization |
| NBSAP | National Biodiversity Strategy and Action Plan |

| | |
|---|---|
| NHC | National Housing Corporation |
| NSSF | National Social Security Fund |
| OSBP | One Stop Border Post |
| PAPU | Pan African Postal Union |
| PPP | Public Private Partnership |
| PSSSF | Public Service Social Security Fund |
| RSF | Rapid Support Forces |
| SADC | Southern African Development Community |
| SAF | Sudan Armed Forces |
| SAMEV | Singapore-Africa Ministerial Exchange Visit |
| SFD | Saudi Fund for Development |
| SGR | Standard Gauge Railway. |
| SUZA | State University of Zanzibar |
| TATO | Tanzania Association of Tour Operators |
| TAZARA | Tanzania-Zambia Railway Authority |
| TCB | Tanzania Commercial Bank |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TICAD | Tokyo International Conference on African Development |
| TICAD-9 | The 9th Tokyo International Conference on African Development |
| TISEZA | Tanzania Investment and Special Economic Zones Authority |
| TMDA | Tanzania Medicines and Medical Devices Authority |
| TNBC | Tanzania National Business Council |

| | |
|---|---|
| TPA | Tanzania Ports Authority |
| TPSF | Tanzania Private Sector Federation |
| UAE | United Arab Emirates |
| UN | United Nations |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UNESCO | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization |
| UNGA | United Nations General Assembly |
| UNHCR | United Nations High Commissioner for Refugees |
| UNICEF | United Nations International Children's Emergency Fund |
| WHO | World Health Organization |
| ZIPA | Zanzibar Investment Promotion Authority |

## VIONGOZI WA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI



**Mhe. *Balozi* Dkt. Mahmoud Thabit Kombo (Mb.)**
Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki



***Mhe. Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe (Mb.)***
Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki



***Mhe. James Kinyasi Millya (Mb.)***
Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki



***Balozi* Dkt. Samwel William Shelukindo**
Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki



***Balozi* Said Shaib Mussa**
Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

## 1.0 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, iliyochambua utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema iliyotuwezesha kukutana hapa leo na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kuwajalia afya njema Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine na watanzania kwa ujumla.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa hii ni hotuba yangu ya kwanza baada ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuniamini na kuniteua tena kuwa Mbunge na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa mara ya pili mimi pamoja na viongozi wenzangu katika Wizara hii, tunatoa shukrani za dhati kwa kuaminiwa na tunaahidi kuendelea kutimiza majukumu yetu kwa weledi, ari, ubunifu, kujituma na kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sera na sheria za

ndani, miongozo mbalimbali, pamoja na mikataba ya Kikanda na Kimataifa ili kuimarisha uhusiano wa kimataifa na kulinda maslahi ya Taifa letu duniani.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba uniruhusu kwa namna ya pekee nimshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanadiplomasia Nambari Moja Nchini kwa kuchaguliwa kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025. Hii imeonesha imani kubwa waliyonayo watanzania juu yake na Serikali anayoiongoza. Tunamuombea afya njema ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kuliongoza Taifa letu.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akila kiapo kuanza kutumikia rasmi nafasi hiyo tarehe 3 Novemba, 2025.*

5. ***Mheshimiwa Spika,*** imani hiyo kubwa imejengwa juu ya namna ambavyo Mheshimiwa Rais ameendelea kuiongoza nchi kwa mafanikio, ikiwemo kulinda na kuimarisha taswira ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kimataifa sambamba na kuimarisha uhusiano wa uwili na nchi mbalimbali, taasisi za kikanda na

kimataifa na kuliletea heshima kubwa Taifa letu. Katika kipindi hiki, Mheshimiwa Rais ameikuza na kuimarisha diplomasia ya Tanzania kwa umahiri wa hali ya juu na kuwezesha kulinda na kutimiza malengo ya kiuchumi ya Taifa letu kama nitakavyoainisha katika hotuba yangu.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa *Balozi* Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naamini uchapakazi wake mahiri utamsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu hususan katika kukuza diplomasia na kuendeleza Uhusiano Kimataifa.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ninamtakia mafanikio makubwa katika kuendelea kuijenga Zanzibar yenye manufaa. Aidha, Wizara itaendelea kuzingatia maslahi na masuala mahsusi ya Zanzibar katika uhusiano wa kimataifa kwa kuzingatia umuhimu wa kipekee wa Muungano wetu kama ilivyoainishwa katika Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), kwa kuaminiwa na Mamlaka na kuidhinishwa na Bunge lako kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ya bajeti ya ofisi yake aliyoiwasilisha kwa umahiri mkubwa. Hotuba hiyo imejenga msingi wa hotuba za bajeti za wizara ikiwemo hotuba yangu ninayoiwasilisha hapa leo.

9. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Musa Azzan Zungu (Mb.), kwa

kuchaguliwa kuwa Spika wa nane (8) wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.), kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uongozi wenu thabiti umelifanya Bunge kuendelea kuwa chombo imara cha kutunga Sheria, kusimamia Serikali na kuwakilisha wananchi kwa ufanisi.

10. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge Mhe. Deodatus Phillip Mwanyika (Mb.), Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb.), na Mhe. Cecilia Paresso (Mb.), kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge hili Tukufu. Juhudi, hekima na maarifa yenu vimeendelea kukipa heshima chombo hiki muhimu mbele ya umma wa watanzania, jumuiya ya kimataifa na kukiwezesha kuisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa napenda kumshukuru Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Makamu Mwenyekiti Mhe. Pascal Inyasi Chinyele (Mb.), na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia na kwa kazi kubwa ya kuishauri Wizara na Serikali kwa ujumla. Miongozo na ushauri wao katika masuala mbalimbali imekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu ambayo wakati wote imekuwa ikisaidia kuboresha mipango na shughuli zinazotekelezwa na Serikali katika kuwahudumia wananchi. Ninaamini mijadala katika Mkutano huu itaendelea kuthibitisha uimara wa Bunge katika kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kuishauri na kuisimamia Serikali kikamilifu.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kuwa wawakilishi wa nchi yetu katika taasisi za kikanda na kimataifa ikiwemo Bunge la Afrika, Bunge la Afrika Mashariki, Jukwaa la Kibunge la SADC, Umoja wa Mabunge Duniani na Jukwaa la Kibunge la nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu. Ninawatakia kila la heri katika kuwakilisha na kutetea maslahi ya nchi katika taasisi hizo na kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na Kimataifa.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Mawaziri wote na viongozi mbalimbali kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi na nyadhifa mbalimbali katika wizara, taasisi, wakala na vyombo vya Serikali. Kwa dhati kabisa, nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao. Nitaendelea kutoa ushirikiano kwao katika kutimiza azma na malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. **Kazi na Utu; Tunasonga Mbele!!**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwaamini na kuwateua Mhe. Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe (Mb.) na Mhe. James Kinyasi Millya (Mb.) kuwa Manaibu Mawaziri katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Napenda kuwashukuru viongozi hao kwa ushirikiano wa dhati wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwaamini *Balozi* Dkt. Samwel William Shelukindo, Katibu Mkuu; na Mhe. *Balozi* Said Shaibu Mussa, Naibu Katibu Mkuu. Aidha, nipende kutumia fursa hii kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Waheshimiwa

Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania Nje ya Nchi, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote kwa ujumla kwa ushirikiano na juhudi zao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumpendekeza Mhe. *Balozi* Stephen Patrick Mbundi, aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki kwenye nafasi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kupitishwa kwa kishindo na Wakuu wote wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wa 25 uliofanyika tarehe 7 Machi, 2026 jijini Arusha. Uwepo wa Mhe. *Balozi* Stephen Mbundi katika Jumuiya hiyo umeipa Heshima ya Juu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa pamoja tunapongeza sana hatua ya kushika nafasi hiyo.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee, napenda kuishukuru familia yangu ikiwemo mke wangu mpendwa kwa upendo, uvumilivu, kuniombea na kunitia moyo wakati ninapoendelea kutekeleza majukumu yangu kwa juhudi na weledi.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kwamba wapo watanzania wenzetu waliofikwa na maafa mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Nitumie fursa hii kuwapa pole watanzania wote waliopoteza ndugu jamaa na marafiki na mali zao kutokana na maafa hayo. Ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu awajalie majeruhi wote uponyaji wa haraka ili waweze kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa letu na aendelee kuwapumzisha kwa amani wale waliopoteza maisha.

## 2.0 MISINGI YA TANZANIA KATIKA UHUSIANO WA KIMATAIFA

20. ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kudumisha misingi ya uhusiano na ushirikiano wa kimataifa, kama ilivyowekwa na waasisi wa Taifa letu na kama ilivyoainishwa katika Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la 2024. Misingi hiyo ni Kulinda Mamlaka kamili ya nchi, mipaka ya nchi na uhuru wa kisiasa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Kulinda uhuru, haki za binadamu, usawa na demokrasia; Kukuza ujirani mwema na Kukuza Umoja wa Afrika.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** misingi mingine ni kuongeza ushirikiano wa kiuchumi na washirika wa maendeleo; kuwezesha utekelezaji wa sera ya kutofungamana na upande wowote na ushirikiano wa nchi zinazoendelea; kuunga mkono Umoja wa Mataifa katika kuimarisha maendeleo ya kiuchumi, amani na usalama; na kulinda maadili, mila, desturi na utamaduni wa watu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Misingi hii imechangia kudumisha heshima na taswira njema ya Taifa letu kupitia ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa.

### Tathmini ya Hali ya Siasa, Ulinzi na Usalama Ulimwenguni

22. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya siasa za ulimwengu imeendelea kudhoofika kutokana na changamoto zinazochangia kukosekana kwa utulivu wa kisiasa katika maeneo mbalimbali. Hali hii imechangia kuongezeka kwa migogoro ya kimataifa ambayo imesababisha vita vya moja kwa moja au vita vya uwakala (*proxy wars*).

23. ***Mheshimiwa Spika,*** migogoro hii inachochewa na ushindani wa maslahi na uwepo wa migogoro ya muda

mrefu inayohusu mipaka ambayo haijapatiwa ufumbuzi wa kudumu, mivutano ya kisiasa kati ya mataifa jirani, pamoja na kuingiliwa kwa masuala ya ndani ya nchi na mataifa ya nje yanayolenga kulinda au kupanua ushawishi wao wa kisiasa na kiuchumi katika maeneo hayo.

**Afrika**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya siasa, ulinzi na usalama barani Afrika imeimarika ikilinganishwa na miongo miwili iliyopita. Hata hivyo, baadhi ya nchi bado zinakabiliwa na migogoro ya kisiasa na kiusalama inayochangiwa na kukosekana kwa misingi imara ya utawala, ushindani wa madaraka na uwepo wa makundi yenye silaha na ushawishi wa mataifa ya nje. Baadhi ya nchi zinazokabiliwa na migogoro hiyo barani Afrika ni pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Sudan, Sudan Kusini, Somalia, Madagascar na Ukanda wa Sahel.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua fursa ya kipekee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Mstaafu Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuteuliwa na Mwenyekiti wa kamisheni ya Umoja wa Afrika kuwa mjumbe Maalum wa Pembe ya Afrika (yaani Horn of Africa) inayojumuisha nchi sita (6).

26. ***Mheshimiwa Spika,*** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za ufumbuzi wa mgogoro huo kwa njia ya amani kupitia IGAD, Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Aidha, Serikali inampongeza na kumtakia kheri Mheshimiwa Dkt. Kikwete katika kutekeleza jukumu hilo muhimu alilopewa. Tuna matumaini kuwa, kutokana na uzoefu wake mkubwa kwenye masuala ya usuluhishi wa

migogoro atatekeleza jukumu hilo kwa weledi na kutimiza matarajio ya Umoja wa Afrika.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** kuteuliwa kwake Mheshimiwa Kikwete katika nafasi hiyo kumeliletea Heshima Kubwa Taifa letu, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye aliridhia na kuidhinisha jina hilo la Mheshimiwa Kikwete kuwasilishwa kwa Mwenyekiti wa kamisheni ya Umoja wa Afrika.

**Mashariki ya Kati**

28. ***Mheshimiwa Spika,*** migogoro Mashariki ya Kati kwa kiasi kikubwa inasababishwa na masuala ya mipaka, usalama, dini na ushindani wa madaraka ambayo imechangia kudhoofisha hali ya ulinzi na usalama katika baadhi ya nchi za ukanda huo. Baadhi ya migogoro iliyojitokeza katika eneo hili ni pamoja na:

**Marekani, Israel na Iran**

29. ***Mheshimiwa Spika,*** mwanzoni mwa mwaka 2026 dunia imeshuhudia mgogoro mkubwa Mashariki ya Kati ukizihusisha nchi za Marekani na Israel dhidi ya Iran. Mizizi ya mgogoro huu ni tangu Mapinduzi ya Iran ya mwaka 1979 yaliyobadilisha nchi hiyo kutoka kuwa mshirika wa karibu wa Marekani na Israel na kuwa mpinzani wa kimkakati wa Sera za Magharibi katika eneo la Mashariki ya Kati. Hatua hii ilijenga uhasama wa muda mrefu wenye mchanganyiko wa masuala ya siasa, usalama na kiitikadi.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa sasa chanzo kikuu cha mvutano unaoendelea kati nchi hizo ni mpango wa nyuklia wa Iran ambapo Marekani na Israel zimekuwa

zikihofia uwezekano wa Iran kupata uwezo wa silaha za nyuklia, huku Iran ikisisitiza kuwa mpango wake ni wa matumizi ya muhimu na ya kawaida ya nishati. Israel na Marekani zimeendelea kuwa na ushirikiano wa karibu wa kiusalama na kijeshi unaolenga kuzuia Iran kuimarisha uwezo wake wa kijeshi, huku Israel ikiona Iran kama tishio la moja kwa moja kutokana na uungaji mkono wake kwa makundi ya upinzani na wapiganaji wa Mashariki ya Kati husussan Hezbollah na Hamas.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua za hivi karibuni, mgogoro uliongezeka na kufikia vita vya moja kwa moja kabla ya kufikiwa kwa makubaliano ya muda ya kusitisha mapigano (*ceasefire*) kupitia upatanishi wa mataifa na mashirika ya kimataifa pamoja na juhudi za kidiplomasia za kupunguza mapigano na kurejesha mazungumzo kuhusu mpango wa nyuklia.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kusitishwa kwa mapigano, hali ya tahadhari inaendelea ambapo pande husika zimeacha mashambulizi ya moja kwa moja huku zikiendelea na misukumo ya kisiasa, kiusalama na kiintelijensia. Pamoja na jitihada zinazoendelea za kidiplomasia, chanzo cha mgogoro bado hakijapatiwa suluhisho la kudumu. Hali hii imeathiri huduma muhimu pamoja na usafiri wa majini, hususan katika Mlango wa Bahari wa Hormuz. Aidha, athari zake zimeonekana kimataifa kupitia kupanda kwa bei za mafuta na nishati, jambo linalochangia mfumuko wa bei, ikiwemo nchini Tanzania.

**Israel na Palestina**

33. ***Mheshimiwa Spika,*** mgogoro kati ya Israel na Palestina umeendelea kuwepo ingawa sio mapigano ya moja kwa moja huku juhudi za kimataifa za kutafuta ufumbuzi zikiendelea. Mazungumzo ya kisiasa kuhusu

suluhisho la mgogoro yameendelea kukwama kutokana na tofauti za msingi kuhusu mipaka, usalama, makazi ya walowezi na hadhi ya Jerusalem, huku Ukanda wa Gaza na baadhi ya maeneo ya Ukingo wa Magharibi yakiendelea kuwa na matukio ya mara kwa mara ya mvutano wa kiusalama na kijeshi. Mgogoro huu umesababisha athari kubwa ikiwemo vifo, uharibifu wa miundombinu ya kijamii kama hospitali, shule na makazi pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wakimbizi na watu waliokosa makazi ya kudumu.

**Yemen**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama ya Yemen bado sio ya kuridhisha licha ya juhudi za upatanishi za kikanda na kimataifa ambapo makubaliano ya kupunguza mapigano yameleta utulivu kiasi lakini mgogoro wa kisiasa kati ya Serikali na wapiganaji wa Kihouthi bado haujatatuliwa kikamilifu. Hali hii inaendelea kuathiri usalama wa Bahari ya Shamu na njia za biashara za kimataifa kutokana na mashambulizi ya mara kwa mara na hatari za usafirishaji.

**Syria**

35. ***Mheshimiwa Spika,*** vita vya wenyewe kwa wenyewe Syria vimepungua baada ya mapinduzi ya Serikali iliyokuwa madarakani, hakuna tena mapigano ya moja kwa moja katika maeneo mengi lakini nchi bado imegawanyika kisiasa na kiusalama huku baadhi ya maeneo yakiwa chini ya udhibiti wa Serikali na mengine yakidhibitiwa na vikundi vya upinzani. Mazungumzo ya kisiasa ya kurejesha umoja wa kitaifa yamekuwa yakisuasua kutokana na mgawanyiko wa maslahi ya mataifa yanayohusika moja kwa moja na vita hivi.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za jumuiya ya kimataifa zakutafuta suluhisho la kudumu la migogoro hiyo yote kwa njia ya amani na mazungumzo ya diplomaisia kwa Mabara yote yote Ulimwenguni kupitia Jumuiya za EAC, SADC, AU na UN.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

37. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara iliweka vipaumbele vifuatavyo:

(i) Kuendelea kuimarisha uratibu na ushirikiano wa uwili pamoja na ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa ili kulinda maslahi ya taifa; kustawisha diplomasia ya kisiasa; na kujenga uhusiano wa karibu na nchi washirika;

(ii) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la 2024 hususan utekelezaji wa diplomasia ya uchumi ikiwemo kukuza upatikanaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi, kuvutia uwekezaji na kukuza utalii;

(iii) Kuongeza ushawishi wa Tanzania kwa nchi nyingine katika masuala mtambuka kwenye Jumuiya na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa kwa maslahi mapana ya Taifa;

(iv) Kushiriki katika jitihada za upatikanaji wa amani, ulinzi na usalama kwa nchi, Jumuiya za Kikanda na Kimataifa; na

(v) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi wa Wizara, kuimarisha utawala bora na rasilimali watu pamoja na kutekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara na Taasisi zake.

## 3.1 Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

### Makusanyo ya Maduhuli

38. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya **shilingi 1,454,426,000** kutokana na vyanzo mbalimbali vilivyopo Makao Makuu ya Wizara na Balozi za Tanzania nje ya nchi. Mapato hayo yanatokana na upangishaji wa nyumba za Serikali zilizopo nje ya nchi na uthibitishaji wa nyaraka mbalimbali. Kati ya fedha hizo, **shilingi 197,500,000** sawa na **asilimia 13.6** ni makisio ya Makao Makuu na **shilingi 1,256,926,000** sawa na **asilimia 86.4** ni makisio ya Balozi za Tanzania Nje ya Nchi.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** kufikia tarehe 30 Aprili 2026, Wizara ilikusanya kiasi cha **shilingi 918,776,947.92** sawa na **asilimia 63.17** ya lengo la mwaka. Aidha, kati ya fedha hizo **shilingi 192,359,002** sawa na **asilimia 20.9** ya makusanyo zilikusanywa Makao Makuu na **shilingi 726,417,945.92** sawa na **asilimia 79.1** ya makusanyo zilikusanywa na Balozi za Tanzania Nje ya Nchi.

### Fedha Zilizoidhinishwa

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliidhinishiwa kiasi **cha shilingi 340,538,614,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi 294,998,588,000** zilitengwa kwa matumizi ya kawaida, ambapo **shilingi 273,661,477,000** ni za matumizi mengineyo na **shilingi 21,337,111,000** ni za mishahara. Mishahara inajumuisha ruzuku ya **shilingi 3,350,066,000** kwa ajili ya mishahara ya Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim.

Aidha, **shilingi 45,540,026,000** zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

41. ***Mheshimiwa Spika***, kadhalika, bajeti ya maendeleo ilijumuisha kiasi cha **shilingi 10,260,000,000** kwa ajili ya kugharamia ujenzi, ukarabati na ununuzi wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi balozini; **shilingi 34,000,000,000** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa makao makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu jijini Arusha; na **shilingi 1,280,026,000** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya mihadhara katika Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim jijini Dar es Salaam.

**Fedha Zilizopokelewa na Kutumika**

42. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2026, Wizara imepokea na kutumia kiasi cha **shilingi 271,316,547,210.19** sawa na **asilimia 79.67** ya bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kati ya fedha hizo, matumizi mengineyo ni **shilingi 249,536,420,050.20** sawa na **asilimia 91.18** ya bajeti ya matumizi mengineyo; mishahara ni **shilingi 17,249,285,516.73** sawa na **asilimia 80.84** ya bajeti ya mishahara na maendeleo ni **shilingi 4,530,841,643.26** sawa na **asilimia 9.95** ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa. Aidha, mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na kupokelewa ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 1** hapa chini.

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Fedha Zilizoidhinishwa, Kupokelewa na Kutumika kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026**

| Na. | Matumizi | Fedha Zilizoidhinishwa (Sh.) | Fedha Zilizopokelewa na Kutumika (Sh.) | Asilimia ya fedha zilizopokelewa na kutumika |
|---|---|---|---|---|
| **A** | **B** | **C** | **D** | **D/C** |
| (i) | Matumizi Mengineyo | 273,661,477,000 | 249,536,420,050.20 | 91.18 |
| (ii) | Mishahara | 21,337,111,000 | 17,249,285,516.73 | 80.84 |
| (iii) | Maendeleo | 45,540,026,000 | 4,530,841,643.26 | 9.95 |
| | **JUMLA** | **340,538,614,000** | **271,316,547,210.19** | **79.67** |

## 3.2 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Kuzingatia Vipaumbele

43. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Wizara iliratibu shughuli zinazolenga kuimarisha ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi nyingine, Jumuiya za Kikanda na Mashirika ya Kimataifa kwa madhumuni ya kudumisha ujirani mwema, kukuza diplomasia na ushirikiano wa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Baadhi ya shughuli zilizofanyika katika eneo hili ni kama ifuatavyo:

### Ushirikiano na Nchi za Afrika

44. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Julai 2025, Wizara iliratibu na kushiriki katika ziara ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchini Comoro ambapo alikuwa Mgeni Rasmi kwenye Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Umoja wa Visiwa vya Comoro. Kupitia wa ziara hiyo, Mheshimiwa Rais aliahidi kupeleka madaktari bingwa wa afya kwa ajili ya kufanyika kwa Kambi ya Matibabu Kisiwani Anjouan.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ahadi hiyo, mwezi Oktoba 2025 ilifanyika Kambi ya Matibabu kisiwani

Anjouan iliyoshirikisha taasisi sita za afya kutoka Tanzania, ambapo wagonjwa takriban 3,600 walipata matibabu ya moja kwa moja na 1,500 walipatiwa rufaa kwa matibabu zaidi nchini Tanzania. Hatua hiyo imechochea ongezeko la wagonjwa kutoka Comoro wanaokuja nchini kwa ajili ya huduma za matibabu ya kibingwa na hivyo kukuza utalii wa tiba.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Julai 2025, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 16 wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano (JPC) kati ya Tanzania na Rwanda, uliyofanyika Kigali, Rwanda. Kupitia Mkutano huo, pande mbili zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya kimkakati na yenye tija hususan, kwenye sekta za uchukuzi, biashara, uwekezaji na mawasiliano. Aidha, Tanzania na Rwanda zilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kwenye Sekta ya Kilimo.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, mwezi Julai 2025, Wizara iliratibu na kushiriki Mkutano wa Sita wa Tume ya Pamoja ya Ulinzi na Usalama (JPCDS) kati ya Tanzania na Msumbiji, uliyofanyika Maputo, Msumbiji. Kupitia Mkutano huo, Tanzania na Msumbiji zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya ulinzi na usalama, ikiwemo mapambano dhidi ya ugaidi.

48. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Agosti 2025, Wizara iliratibu na kushiriki katika uzinduzi wa ujenzi wa kipande cha reli ya kisasa (SGR) cha Uvinza kwa Tanzania hadi Musongati kwa Burundi yenye urefu wa Kilometa 282, uliofanyika nchini Burundi, ambapo ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi huo utakapokamilika utachochea shughuli za kiuchumi pamoja na kuimarisha mtangamano wa kikanda.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, mwezi Agosti 2025, Wizara iliratibu ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Kanali (Mstf.) Kembo Campbel Mohadi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe, iliyofanyika nchini. Ziara hiyo imeimarisha uhusiano kati ya Tanzania na Zimbabwe kwa kutambua na kuenzi mchango wa Tanzania kwenye harakati za ukombozi wa Taifa la Zimbabwe na Bara la Afrika kwa ujumla ambapo umuhimu wa kuhifadhi kumbukumbu za harakati za ukombozi nchini ulisisitizwa.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi 2026, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Tano wa Tume ya Pamoja ya Kudumu (JPC) kati ya Tanzania na Uganda, uliofanyika Jijini Dar es Salaam. Katika Mkutano huo, pande mbili zilikubaliana kuimarisha ushirikiano kwenye masuala ya Diplomasia, Ulinzi na Usalama; Nishati; Uchukuzi; Miundombinu; Uhamiaji; Kilimo; Viwanda na Biashara. Kupitia Mkutano huo, pande mbili zilisaini Hati ya Makubaliano (MoU) kuhusu uendelezaji wa mradi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Isaka-Lusahunga-Murongo nchini Tanzania hadi Kikagati-Mpondwa nchini Uganda.

**Ushirikiano na Nchi za Asia na Australasia**

51. ***Mheshimiwa Spika***, kasi ya mabadiliko ya siasa za kikanda duniani yameifanya Tanzania kuongeza juhudi za kujipambanua kama mshirika wa kimkakati na wa kuaminika katika nyanja za nishati mbadala, usalama wa chakula na uchumi wa kidijitali. Wizara imefanikiwa kuratibu ziara za ngazi za juu, mikutano ya kisekta, na programu za kujenga uwezo kwa Watanzania ambazo zimeimarisha nafasi ya Tanzania katika mnyororo wa thamani wa kimataifa ikiwemo katika eneo la Asia na Australasia.

52. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Agosti 2025, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Tisa wa Ngazi ya Mawaziri wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika (TICAD-9) uliofanyika jijini Yokohama, Japan. Katika Mkutano huo, Serikali ya Japan ilitangaza mpango wa kushirikiana na nchi za Afrika katika maeneo ya Ulinzi, Uchumi na Maendeleo ya Jamii.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa mafanikio ambayo Tanzania imeyapata katika utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano wa TICAD 9, ni pamoja na upatikanaji wa boti za doria za kisasa zilizogharimu **Dola za Marekani milioni 1.6** chini ya ufadhili wa Serikali ya Japan kupitia kampuni ya YAMAHA kwa kushirikiana na UNDP. Hii ni sehemu ya utekelezaji wa awamu ya pili ya Mradi wa Kuimarisha Usalama wa Mwambao wa Bahari ya Hindi utakaogharimu kiasi cha **Dola za Marekani milioni 2.21**. Aidha, kiasi kilichobaki kitatumika kufadhili mafunzo ya shughuli za kiuchumi kwa wanawake; ununuzi wa mashine za kusagia mwani; na ujenzi wa makaushio ya mwani katika Wilaya ya Kilindi Mkoani Tanga.

54. ***Mheshimiwa Spika***, nchi ya Japan imeendelea kufadhili utekelezaji wa mradi wa *The Economic and Social Development Programme* (ESDP) wenye thamani ya kiasi cha Yen za Japan milioni 350 sawa na takribani **Dola za Marekani milioni 2.6**. Programu hiyo imejumuisha ununuzi wa meli ya kwanza ya uvuvi katika bahari kuu ijulikanayo kwa jina la *TAFIVO FV.01* ambayo itatumika katika uvuvi wa samaki aina ya Tuna na jamii zake; pamoja na ununuzi wa kiwanda cha kutengeneza barafu, vifaa vya uvuvi, kusimika miundombinu ya kuhifadhi bidhaa baridi.

55. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya kijamii inayofadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia program inayofahamika

kama *Grant Assistance on Grassroots Human Security Projects (GGHSP)* inayosimamiwa na Ubalozi wa Japan hapa nchini. Kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026, jumla ya miradi 32 imetekelezwa katika mikoa ya Lindi, Iringa, Njombe, Tabora, Arusha, Ruvuma, Dar es Salaam, Pwani, Kigoma, Kagera, Geita, Mbeya, Mtwara, Tanga, Mara, Katavi, Simiyu na Arusha. Utekelezaji wa miradi hiyo umeboresha huduma za kijamii na hivyo kuiweka Tanzania katika nafasi nzuri ya kuendelea kunufaika zaidi na programu hiyo katika kipindi kijacho.

56. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Wizara imeratibu makubaliano ya ufadhili wa utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Matibabu ya Ugonjwa wa Figo na Upandikizaji pamoja na upatikanaji wa mashine ya kisasa ya *Digital Substraction Angiography (DSA)* katika Hospitali ya Benjamin Mkapa. Mradi huo utagharimu Yen za Japan bilioni 1.5 utakaofadhiliwa na Taasisi ya *Tokushukai Medical Corporation* ya Japan. Kituo hicho kitasaidia kuboresha huduma za tiba za figo hapa nchini, kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya, na kuendeleza tafiti za pamoja katika magonjwa ya figo na upandikizaji. Kukamilika kwa mradi huo kutapunguza gharama na changamoto za wagonjwa kusafiri nje ya nchi kwa matibabu.

57. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Agosti 2025, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Tano wa Mawaziri wa Afrika na Singapore (5$^{th}$ SAMEV) na Jukwaa la Nane la Biashara kati ya Afrika na Singapore (8$^{th}$ ASBF). Ujumbe ulihusisha viongozi kutoka *TPSF, TNBC, TISEZA, TCB, PSSSF* na wafanyabiashara katika sekta za madini, usafirishaji, uzalishaji bidhaa, fedha, kilimo na mazingira. Kupitia Mkutano huo, Tanzania ilitangaza fursa za uwekezaji kwa viongozi wa biashara zaidi ya 700 kutoka Bara la Asia na Afrika.

58. ***Mheshimiwa Spika***, katika mazungumzo ya pande mbili na Mhe. Dkt. Vivian Balakrishnan, Waziri wa Mambo ya Nje wa Singapore, tulikubaliana kuongeza kasi ya ushirikiano kati ya Tanzania na Singapore katika diplomasia, biashara, uwekezaji, usimamizi wa mazingira na maendeleo ya rasilimali watu. Aidha, tulikubaliana kuharakisha majadiliano ya Mkataba wa Kuzuia Utozaji Kodi Mara Mbili (*Double Taxation Agreement*) na Mkataba wa Kukuza na Kulinda Uwekezaji (*Bilateral Investment Promotion and Protection Agreement*), pamoja na makubaliano ya kufanya mashauriano ya kisiasa, uwezeshaji wa biashara, biashara ya kaboni, kujengea uwezo viongozi wa umma na utalii. Tunatarajia makubaliano hayo yatakamilika mwaka huu mwezi Juni 2026 na utekelezaji wake kuanza kwa wakati.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Oktoba 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hafla ya uzinduzi na Makabidhiano ya Mradi wa Ujenzi wa Makumbusho ya Kisasa ya Hifadhi ya Jiolojia ya Ngorongoro – Lengai (*Urithi Geo- Meseum*) iliyopo mkoani Arusha. Mradi huo wenye thamani ya **RMB 90,350,000** sawa na takriban **shilingi bilioni 32**, ni kichocheo muhimu cha ushirikiano kupitia sekta ya utalii na maliasili kati ya Tanzania na China. Makumbusho hiyo inatarajiwa kuwa kichocheo kikubwa cha kuongeza idadi ya watalii kutoka Jamhuri ya Watu wa China na mataifa mengine.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa *Balozi* Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipomwakilisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uzinduzi wa Mradi wa Ukarabati wa

Miundombinu ya Reli ya TAZARA uliofanyika jijini Lusaka, Zambia.

61. ***Mheshimiwa Spika***, uwekezaji katika mradi huo utagharimu kiasi cha **Dola za Marekani bilioni 1.4** sawa na takriban **shilingi trilioni 3.4** ambapo utahusisha ukarabati mkubwa wa miundombinu ya reli, vituo vya abiria na mizigo na mfumo wa mawasiliano ya reli ikiwemo ununuzi wa vichwa vya treni, mabehewa ya abiria na mizigo. Mradi huo utakapokamilika, utaongeza ufanisi wa TAZARA na kuhamasisha ukuaji wa uchumi kwa ujumla kupitia ushoroba wa uchukuzi wa TANZAM baina ya Tanzania na nchi za SADC.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha uhusiano wa watu kwa watu ambapo Watanzania wameweza kunufaika na fursa za mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa nafasi 800 zilizotolewa na China kwa Tanzania. Hatua muhimu zinazochukuliwa na Wizara ni kuhakikisha upatikanaji wa viza ya kuingia nchini China unarahishwa ili kuwezesha wanafunzi na watumishi wa umma pamoja na sekta binafsi kuendelea kuimarisha ushirikiano huo wa watu kwa watu na hivyo kuchochea ukuaji wa biashara, utalii na uwekezaji.

63. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Januari 2026, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Wang Yi, Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti na Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Watu wa China aliyefanya ziara rasmi nchini Tanzania. Kupitia ziara hiyo, Tanzania ilishawishi kupata msamaha wa deni la **RMB millioni 100 (Takriban shilingi bilioni 34)** ambalo ni mkopo usiokuwa na riba uliofadhili ujenzi wa Ofisi Ndogo ya Wizara iliyopo jijini Dar es Salaam. Msamaha huo umepunguza mzigo mkubwa wa kifedha kwa Serikali.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** ziara hiyo imekuwa chachu ya kuimarisha ushirikiano wa kimkakati katika sekta za

kipaumbele ikiwemo biashara, uwekezaji, miundombinu na nishati. Kupitia ziara hiyo, Serikali ya China iliahidi kuendelea kufadhili miradi ya maendeleo nchini ikiwemo ile iliyo chini ya mpango wa Jukwaa la FOCAC. Katika miradi hiyo, ipo ya mikopo yenye masharti nafuu iliyo kwenye hatua za majadiliano. Hali kadhalika, ipo miradi ya msaada ambapo baadhi iko katika hatua ya kuanza utekelezaji kama vile Mradi wa Teknolojia ya kuandaa malisho ya mifugo na samaki (*China – Aid JUNCAO Technical Aid*) na mradi wa madaktari bingwa wa kujitolea ambapo tayari Kundi Na. 28 lenye madaktari 15 kutoka China wamewasili nchini Aprili, 2026 kwa ajili ya kutoa huduma kwenye hospitali za Serikali kwa kipindi cha miaka miwili.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, kupitia ziara hiyo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China iliunga mkono dhamira ya Tanzania kuwania nafasi ya Mjumbe asiye wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa kipindi cha 2029-2030.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Korea kupitia mfuko wa *Economic Development Cooperation Fund* (EDCF) ambapo Korea iliridhia kuipatia Tanzania mkopo nafuu wa **Dola za Marekani bilioni 2.5** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Serikali ya Jamhuri ya Korea imeidhinisha miradi minne kwa ajili ya utekelezaji ikijumuisha uendelezaji wa Hospital ya Taifa ya Muhimbili; ujenzi wa Hospitali ya Binguni Zanzibar; ujenzi wa bandari ya uvuvi ya Bagamoyo na ujenzi wa chuo cha reli, Dodoma.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano wa ufuatiliaji uliofanyika mwezi Novemba 2025, Serikali ya Korea ilitangaza kuitambua Tanzania kuwa miongoni mwa nchi tano za kipaumbele katika ushirikiano wa maendeleo barani Afrika kwa kipindi cha miaka mitano (2026-2030).

Kutambuliwa huko kunadhihirisha imani kubwa ya Serikali ya Korea kwa Tanzania kutokana na mazingira mazuri ya uwekezaji, utulivu wa kisiasa na mafanikio ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, Wizara iliratibu ziara ya wafanyabiashara wa Jumuiya ya Waagizaji Bidhaa wa Korea (KOIMA) walioitembelea Tanzania. Miongoni mwa mafanikio yaliyofikiwa ni kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano kati ya KOIMA na Shirikisho la Sekta Binafsi Tanzania (TPSF).

69. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Agosti 2025, Wizara ilifanikiwa kushawishi ujio wa vyombo vya Habari mashuhuri kutoka nchini Korea wakiambatana na wabunge wanne kutoka katika Bunge la Jamhuri ya Korea. Vyombo hivyo vya habari vilitembelea miradi mikubwa iliyokamilika kwa ushirikiano na Benki ya Maendeleo ya Korea (*Korea Exim Bank*), ikiwemo mradi wa Daraja la Tanzanite na ujenzi wa Hospitali ya Mloganzila. Ujumbe huu ulivutiwa na utekelezaji wa miradi hii na kuahidi kuendelea kuitetea Tanzania kuendelea kupata misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Serikali ya Jamhuri ya Korea.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Mei 2026, Wizara iliwezesha upatikanaji wa ridhaa kutoka Serikali ya Indonesia ya kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Ukarabati wa Kituo cha Mafunzo kwa Wakulima Vijijini cha Mikindo ***(Famer's Agriculture and Rural Training Center - FARTC)*** unaofadhiliwa na Serikali hiyo. Kufuatia mkutano wa Nne (4) wa Tume ya Ushirikiano katika Sekta ya Kilimo (*Joint Agriculture Cooperation Committee – JACC)* Serikali ya Indonesia imeeleza kuridhika na utekelezaji wa mradi huo ambao hadi sasa Serikali hiyo imeshatoa kiasi cha **Dola za Marekani 219,049.60** na imeahidi kuendelea kutoa ufadhili ili kukamilisha mradi huo. Aidha, Wizara imeratibu na kusimamia upatikanaji wa nafasi za ufadhili

wa masomo kwa Watanzania kutoka Serikali ya Indonesia ambayo yanafahamika kama ***Kemitraan Negara Berkembang (KNB)*** na ***The Indonesia Aid Scholarship (TIAS***). Kufuatia juhudi hizo, mwezi Aprili 2026, jumla ya Watanzania 310 wamefanikiwa kuingia kwenye orodha ya wanaoweza kunufaika na ufadhili huo.

71. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Aprili 2026, niliongoza ujumbe wa Tanzania kwenye Mkutano wa 9 wa Bahari ya Hindi uliofanyika nchini Mauritius. Katika mkutano huo, Tanzania iliungana na nchi nyingine 13 zilizopo katika Mwambao wa Bahari na kuazimia kuimarisha ushirikiano katika masuala ya usalama wa bahari (*maritime security*); usalama wa nishati (*energy security*); ushirikiano wa kiuchumi hususan katika Uchumi wa Bluu; na kulinda mazingira ya bahari, ili kukabiliana na changamoto zinazotokana na machafuko katika Mashariki ya Kati.

72. ***Mheshimiwa Spika***, katika mkutano huo, Tanzania ilihimiza nchi hizo kuwezesha biashara hususan kwa nchi zisizokuwa na bahari; kushirikiana kwenye kukabiliana na mimea haribifu ya bahari; kulinda usalama wa chakula hususan kwa jamii zinatotegemea bahari kwa chakula; pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kikanda, ili kuwezesha nchi yetu kunufaika ipasavyo na nafasi yetu ya kijiografia.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, Wizara iliwezesha upatikanaji wa viungo bandia kutoka Taasisi ya BMVSS ya nchini India inayojihusisha na utengenezaji wa viungo hivyo. Taasisi hiyo kupitia programu ya *Jaipur Foot Artificial Limb Fitment Camp* kwa kushirikiana na Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI) iliendesha kambi ya kutoa viungo bandia kwa Watanzania waliokuwa na uhitaji ambapo watanzania 600 walipatiwa viungo hivyo ikiwemo miguu na mikono bila malipo na hivyo kuwawezesha

kuendelea na shughuli zao za kujikimu maisha kwa wepesi.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile mwezi Machi 2026, niliongoza maadhimisho ya Siku ya Programu ya Mafunzo ya Kiufundi na Kiuchumi ya India (*ITEC Day*) yaliyofanyika Dar es Salaam. Kwa mwaka huu, kupitia programu ya ITEC nchi yetu imeshanufaika na nafasi za mafunzo ya muda mfupi zipatazo 775 na nafasi za mafunzo ya muda mrefu zipatazo 135 kwa ufadhili wa Serikali ya India. Aidha, Wizara imeweza kupata fursa nyingine za mafunzo zipatazo 30 kutokana na majadiliano kati ya Wizara yangu na Wizara ya Mambo ya Nje ya India yaliyofanyika wakati wa mkutano wa *Raisina Dialogue* mwezi Machi 2026.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Julai 2025, Wizara iliratibu Kongamano la Biashara kati ya India na Zanzibar. Kongamano hili lilihusisha majadiliano ya wafanyabishara kutoka sekta za Umma na Sekta Binafsi wakiwemo wataalam kutoka serikalini, sekta binafsi, wawekezaji, wajasiriamali, na washirika wa maendeleo. Kongamano hilo limewezesha kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano kati ya shirika la *Marketing Assisstance and Reserch Support (MARs)* na Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), hatua itakayochochea uwekezaji kutoka India, kufanikisha maonesho ya pamoja ya uwekezaji na kuimarisha Ushirikiano.




*Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Zanzibar na India lililofanyika mjini Zanzibar mwezi Julai, 2025.*

**Ushirikiano na Nchi za Mashariki ya Kati**

76. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Agosti 2025, Wizara kwa kushirikiana na sekta ya mifugo iliwezesha kuondolewa kwa zuio la usafirishaji wa nyama kutoka Tanzania lililosababishwa na uwepo wa ugonjwa wa mguu na mdomo (*Foot and Mouth Disease - FMD*). Zuio hili lilipelekea changamoto kubwa kwa wafanyabiashara wa Tanzania wanaosafirisha na kuuza nyama katika nchi za Mashariki ya Kati ikiwemo Qatar.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Ubalozi wetu nchini Qatar, tumefanikisha kufunguliwa kwa soko hilo kwa kuzingatia masharti na taratibu zilizoanishwa na mamlaka za nchi hiyo kuanzia mwezi Machi 2026.

78. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Oktoba 2025, Wizara iliratibu na kushiriki katika mazungumzo kati ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Salim bin Mohammed, Waziri wa Mambo ya Kale na Utalii wa Oman. Wakati wa mazungumzo hayo Mhe. Salim alionesha dhamira ya dhati ya kuimarisha ushirikiano wa kihistoria uliopo kati ya Zanzibar na Oman, na kutoa mwelekeo mpya wa ushirikiano katika sekta za utalii, utamaduni na urithi wa kihistoria ambazo ni muhimu kwa ustawi wa kiuchumi na kijamii.

79. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Desemba, 2025, niliwasilisha ujumbe maalum wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenda kwa Muadham Saliman bin Abdulaziz Al Saud Mfalme wa Saudi Arabia, Mtukufu Sheikh Mohammed bin Zayed Al Nahyan, Rais wa Umoja wa Falme za Kiarabu na kwa Mheshimiwa Haitham bin Tariq, Sultan wa Oman. Ziara hizo zimeimarisha ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi hizo.

80. ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuanzishwa kwa majadiliano ya ushirikiano na kampuni ya *Oman Lens Llc* kuhusu Teknolojia ya Akili Unde (AI) na Satelaiti za Uchunguzi wa Dunia. Aidha, Tanzania na Oman zilikubaliana kuanzisha Kongamano la Biashara na kuandaa mkakati wa ushirikiano wa miaka miwili. Hatua hizi zinaongeza fursa za uwekezaji na biashara baina ya pande mbili.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Januari 2026, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mhe. Deus Clement Sangu (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, kushiriki katika Mkutano wa Tatu wa Soko la Ajira Duniani (GLMC 2026), uliofanyika Riyadh, Ufalme wa Saudi Arabia. Ziara hiyo imefungua fursa na kuimarisha ushirikiano katika masuala ya ajira, mafunzo

ya ufundi stadi, uhamaji wa wafanyakazi na ufadhili wa masomo kupitia makubaliano ya pande mbili.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii (Bodi ya Utalii Tanzania), na wadau wa Utalii kutoka Sekta binafsi, Tanzania ilishiriki kwenye Maonesho ya Utalii ya nchini Qatar ambapo Tanzania ilipata fursa ya kukutana na wadau wa Kimataifa wa Utalii na kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania. Kufuatia ushiriki huu, mwezi Januari 2026 Tanzania ilipokea ujumbe wa kampuni kumi za Wakala wa Utalii na Usafiri kutoka Qatar. Hatua hii, inategemewa kuongeza idadi ya watalii kutoka nchini Qatar na maeneo mengine ya Mashariki ya Kati na hivyo kuongezea mapato ya nchi yatokanayo na utalii.

## Ushirikiano na Nchi za Ulaya na Amerika

83. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Julai 2025, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Randeep Sarai, Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa wa Canada hapa nchini. Mheshimiwa Sarai alitembelea miradi ya ushirikiano wa maendeleo katika sekta za Elimu na Afya inayofadhiliwa na Serikali ya Canada. Aidha, wakati wa ziara hiyo Mheshimiwa Sarai alizindua miradi miwili katika sekta ya elimu inayohusisha masuala ya lishe kwa shule za msingi kwa mikoa ya Lindi na Mtwara.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Mheshimiwa Sarai alikutana na kufanya mazungumzo na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambapo walijadiliana kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo utekekelezaji wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na Canada katika sekta ya afya, elimu na uchumi wa Buluu.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Julai 2025, Wizara pia iliratibu na kushiriki katika ziara ya Mheshimiwa Dkt. Constantinos Kombos, Waziri wa Mambo ya Nje wa Cyprus na Mwakilishi wa Umoja wa Ulaya, ambapo Tanzania na Cyprus zilisaini Hati mbili za Makubaliano (MoUs) za kukuza ushirikiano katika sekta za biashara, kilimo, uchumi wa buluu, utalii na uwekezaji kwenye sekta ya madini.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Julai 2025, Wizara iliratibu na kushiriki ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Belaruse. Katika ziara hiyo Tanzania na Belarus zilisaini Mkataba mmoja kuhusu kukuza uhusiano wa kibiashara na Hati tatu za Makubaliano zinazolenga kuimarisha ushirikiano katika maeneo ya uwekezaji, siasa, kilimo na elimu.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Septemba 2025, nilimwakilisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hafla ya uzinduzi wa kituo kipya cha *ODI Global*, taasisi ya tafiti za kimataifa na uchambuzi wa sera nchini Uingereza. Taasisi hiyo imetoa mchango katika maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuhudhuria hafla hiyo, nilishiriki mikutano na taasisi za kifedha, uwekezaji, na mashirika ya kimataifa iliyolenga kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na Uingereza. Aidha, nilifanya mazungumzo na Makatibu Wakuu wa Shirika la Bahari Duniani na Jumuiya ya Madola ambapo tulikubaliana kuimarisha ushirikiano katika sekta za mazingira, nishati safi, kilimo, utalii, teknolojia, biashara, uwekezaji na ufadhili wa miradi ya maendeleo.

89. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Septemba 2025, Wizara iliratibu na kushiriki ziara ya Mheshimiwa Péter Szijjártó,

Waziri wa Mambo ya Nje na Biashara wa Hungary hapa nchini ambapo alizindua rasmi Ofisi ya Ubalozi wa Hungary jijini Dar es Salaam kufuatia kufungwa kwa Ubalozi na Ofisi ya biashara tangu mwaka 1990. Hatua hiyo ilijenga msingi wa kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na kiuchumi kati ya Tanzania na Hungary. Kupitia ziara hiyo Tanzania na Hungary zilisaini Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Kituo cha Kidijitali cha Tanzania na Kampuni ya MeOut kuhusu masuala ya ubunifu.

90. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Septemba 2025, Wizara iliratibu na kushiriki ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Philipo Isdor Mpango aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Marekani ambapo pamoja na masuala mengine alishiriki katika Jukwaa la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Marekani. Kupitia Jukwaa hilo, Taasisi ya *The U.S. International Development Finance Cooperation* iliipatia Tanzania msaada wa Dola za Marekani milioni 300 kupitia Benki ya CRDB kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya.

91. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Desemba 2025, niliongoza ujumbe wa Tanzania kushiriki katika Mkutano wa Pili wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa nchi za Afrika na Urusi uliofanyika nchini Misri. Tanzania ilitumia Mkutano huo kutangaza fursa za uwekezaji na biashara ambapo ilifanikiwa kupata Dola za Marekani milioni 20.5 kutoka Urusi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kilimo, nishati, na elimu.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Aprili 2026, Wizara iliratibu ziara ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Belarus nchini, iliyowezesha kusainiwa kwa Hati za Makubaliano kati ya Kituo cha Taifa cha Kukuza Mauzo ya Nje cha Belarus na Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania pamoja na Shirikisho la Sekta Binafsi Tanzania. Hatua hiyo itachochea kukuza

biashara na uwekezaji na kuimarisha ushirikiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na Belarus.

## Ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya za Kikanda

93. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania kwenye majadiliano ya Jumuiya za Kikanda ambazo nchi yetu ni mwanachama, hususan Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Umoja wa Afrika. Aidha, imeratibu ushiriki wa Tanzania katika utekelezaji wa Itifaki, maazimio na programu za maendeleo za Jumuiya za Kikanda na Mashirika ya Kimataifa kama ifuatavyo:

## Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)

94. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika utekelezaji wa hatua za mtangamano na programu za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika maeneo ya Biashara, Uwekezaji na Sekta za Uzalishaji; Miundombinu ya Kiuchumi na Huduma za Kijamii; pamoja na Siasa, Ulinzi na Usalama. Jitihada hizi zililenga kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa ajenda za Jumuiya.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi 2026, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 25 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika jijini Arusha. Pamoja na masuala mengine, mkutano huo ulijadili Taarifa ya mwaka ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya.

96. ***Mheshimiwa Spika*** katika mkutano huo, ripoti mbalimbali ziliwasilishwa kuhusu utekelezaji wa maamuzi na maagizo ya Wakuu wa Nchi, mfumo endelevu wa uchangiaji wa bajeti na hali ya uchangiaji wa bajeti ya

uendeshaji wa Jumuiya, maendeleo ya rasimu ya Katiba ya Fungamano la Kisiasa, kuridhia na kusaini miswada ya sheria iliyopitishwa na Bunge la Afrika Mashariki pamoja na uteuzi wa Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa Jumuiya.

97. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia Mkutano huo, Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya kwa kipindi cha mwaka mmoja. Aidha, Mkutano ulimteua Mheshimiwa *Balozi* Stephen Patrick Mbundi wa Tanzania kuwa Katibu Mkuu mpya wa Jumuiya kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe 25 Aprili 2026. Kuteuliwa kwa Mheshimiwa *Balozi* Mbundi ni ishara ya kuaminika kwa Tanzania katika Jumuiya za Kikanda.

98. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha ufanisi wa ulipaji wa michango ya uendeshaji wa Jumuiya, Wakuu wa Nchi waliidhinisha mfumo mpya wa uchangiaji wa bajeti unaogawa mchango kwa **asilimia 50** sawa kwa kila Nchi Mwanachama na **asilimia 50** kulingana na Pato la Taifa. Aidha, kwa kutambua hali halisi ya uchumi wa Nchi Wanachama na kuwapunguzia mzigo Nchi Wanachama wenye madeni ya michango, Mkutano wa 25 wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya, uliamua kusamehe **asilimia 50** ya madeni yote ya michango inayozidai Nchi Wanachama kwa sharti kwamba **asilimia 50** iliyobaki ilipwe ndani ya kipindi cha miaka miwili kuanzia tarehe 7 Machi 2026.

99. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine ya kuongeza ufanisi na uwajibikaji wa Nchi Wanachama, Wakuu wa Nchi waliamua kuwa mishahara na posho za Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA) ilipwe na Mabunge ya Nchi zao husika kuanzia Desemba 2027 baada ya kumalizika kwa muda wa Bunge la sasa. Hatua hii itaondoa mzigo kwa Tanzania na nchi nyingine zinazolipa michango yake kwa wakati.

100. ***Mheshimiwa Spika***, aidha, Mkutano wa 25 wa Wakuu wa nchi za Jumuiya umeelekeza Baraza la Mawaziri na Nchi Wanachama kushughulikia na kutatua vikwazo vyote vya biashara visivyo vya kodi vilivyoripotiwa ndani ya Jumuiya ifikapo tarehe 30 Juni 2026.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuongoza wadau wa ndani katika utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaolenga kukuza biashara, kuongeza ufanisi katika uzalishaji, kukuza uwekezaji wa ndani baina ya nchi wanachama na kuendeleza viwanda. Kutokana na mafanikio ya utekelezaji huo, biashara miongoni mwa Nchi Wanachama imeongezeka licha ya changamoto zinazoendelea katika uchumi wa dunia.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** mathalan, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliongezeka kutoka **Dola za Marekani bilioni 1.1605** mwaka 2024 hadi **bilioni 1.2256** mwaka 2025, na thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi wanachama ilipanda kutoka **Dola za Marekani milioni 527.3** hadi **milioni 582.2** katika kipindi hicho.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kuwa na urari chanya wa biashara baina yake na nchi za Jumuiya. Hali hii inafanya soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa miongoni mwa masoko ya kimkakati kwa Tanzania katika kupunguza nakisi ya biashara ya kimataifa.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwezesha biashara na kuondoa vikwazo vya biashara vya kiufundi (*technical barriers to trade*), Jumuiya imeendelea kuwianisha viwango vya ubora wa bidhaa na vipimo. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya viwango 52 vya ubora viliwianishwa na kupitishwa ili kutambuliwa kama viwango vya ubora vya Jumuiya. Miongoni mwa viwango

vilivyowianishwa ni vya mazao ya mahindi, maharage, mchele, vilainishi vya magari na mitambo.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** uwianishaji wa viwango unaondoa vikwazo vya biashara vya kiufundi ambavyo vingetokana na kila nchi kuwa na viwango vyake huku jumuiya ikidhibiti ubora wa bidhaa zinazozalishwa na kuuzwa ndani ya Jumuiya ili kuboresha hali ya maisha, kulinda afya ya walaji, kukidhi viwango vya soko la kimataifa, kuhamasisha biashara na uwekezaji pamoja na kulinda thamani ya fedha.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukuza viwanda, kuhamasisha uzalishaji wa ndani na uhawilishaji wa teknolojia, Jumuiya ina utaratibu wa kutoa unafuu wa kodi (*duty remission*) kwa wazalishaji wa ndani wenye kutumia malighafi au bidhaa za kati ambazo hazipatikani au hazitoshelezi ndani ya Jumuiya. Katika kipindi hiki, Wizara iliratibu uwezeshaji wa wazalishaji 302 wa Kitanzania kunufaika na unafuu wa kodi unaotolewa na Jumuiya kupitia Kanuni ya 4(4) ya Kanuni za Jumuiya ya Afrika Mashariki za Usimamizi wa Forodha kuhusu Misamaha ya Kodi (*EAC Duty Remission Regulations, 2008).*

107. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa makundi ya wazalishaji yaliyonufaika na unafuu huo wa kodi ni viwanda vya kuzalisha nyaya za umeme, sabuni, mafuta ya kulainisha mitambo, waundaji wa pikipiki na bajaji, karatasi na maboksi, vitabu vya shule, nyavu za uvuvi, karatasi za mashine za kielektroniki (EFD), nepi na taulo za kike, betri za Lithium-ion, sukari kwa matumizi ya viwandani, viwanda vya nguo, viwanda vya kuzalisha viatu na waundaji wa meli. Hatua hii imelenga kuimarisha uzalishaji wa ndani katika sekta mbalimbali na kuongeza ushindani wa bidhaa zinazozalishwa nchini katika soko la ndani na nje ya Jumuiya.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa Kikanda wa kuimarisha biashara, kukuza mauzo ya nje na kuongeza thamani katika minyororo wa mazao (*EAC MARKUP II – Market Access Upgrade Programme*). Mradi huu umejikita katika mazao ya kahawa, kakao, viungo, ngozi, na mazao ya bustani. Mradi huu una thamani ya **Euro Milioni 40** sawa na takribani **shilingi bilioni 122** na unatekelezwa katika nchi za Burundi, Kenya, Rwanda, Sudani Kusini, Tanzania na Uganda. Kwa upande wa Tanzania mazao yaliyolengwa ni Kahawa; viungo vya chakula; vifungashio na bidhaa za ngozi.

109. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hiki, shughuli zilizotekelezwa nchini na mradi ni pamoja na kuboresha mazingira ya Biashara ya kahawa kwa kuwezesha kupunguza taratibu za mauzo nje kutoka 44 hadi 30 na lengo ni kupunguza hadi 19. Kupungua kwa taratibu hizi kumewezesha kupunguza gharama za kufanya Biashara pamoja na muda wa kupata vibali husika. Aidha, kampuni ndogo na za kati zipatazo 20 zimepata mafunzo kuhusu masuala ya viwango vya ubora, mbinu za kuchakata zao la kahawa na kuongeza ubora na ushindani. Mafunzo hayo yanajumuisha namna bora ya kufungasha kahawa, uboreshaji wa mikakati ya masoko na matumizi ya mtandao.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Desemba 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Maonesho ya 25 ya wajasiriamali wadogo na wa kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (JuaKali/NguvuKazi) yaliyofanyika Nairobi, Kenya, yaliyoshirikisha wajasiriamali 271 kutoka Tanzania wakiwemo wanaume 45 na wanawake 226. Bidhaa zilizouzwa zilijumuisha nguo, bidhaa za kilimo kama viungo vya chakula, ungalishe, unga wa nafaka, mvinyo, asali, ngozi, tibalishe na korosho, bidhaa za

ufundi, sanaa za uchoraji, pamoja na bidhaa za baharini kama mwani, samaki na dagaa.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki wa wajasiriamali kutoka Tanzania kwenye maonesho hayo uliwawezesha kutangaza bidhaa zao, kupanua soko, na kujenga mtandao wa ushirikiano na wajasiriamali kutoka nchi nyingine wanachama. Aidha, uliwapa ujuzi na uzoefu kuhusu biashara ya mipakani, pamoja na mbinu za ubunifu za kutumia fursa za kibiashara katika mtangamano wa Jumuiya.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia maonesho hayo, Tanzania ilitangazwa mshindi wa jumla wa Maonesho ya 25 ya Wajasiriamali ya EAC ambapo KAYPEE Motors ilishinda kipengele cha Mjasiriamali Bora wa Afrika Mashariki kutokana na uwezo wake wa kutunza mazingira. Napenda kuipongeza kampuni hiyo kwa uwekezaji wake unaozalisha ajira na kuitangaza Tanzania kikanda na kimataifa pamoja na kuwahimiza Watanzania, hususan wanawake na vijana, kuendeleza ubunifu katika uzalishaji wa bidhaa na huduma zenye ushindani ili kutumia ipasavyo fursa za soko la Afrika Mashariki.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Agosti 2025, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano Maalum wa Pamoja wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika kwa njia ya Mtandao. Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, aliyekuwa Makamu wa Rais aliongoza ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo. Mkutano ulipokea na kujadili taarifa ya Mkutano wa Wenyeviti wenza wa EAC-SADC ikiwa ni utekelezaji wa maamuzi ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika mwezi Machi 2025.

114. ***Mheshimiwa Spika***, Mkutano huo uliidhinisha nyaraka zifuatazo; Mwongozo wa namna ya kuunganisha

mchakato wa Nairobi na ule wa Luanda ili kuwezesha mazungumzo ya kidiplomasia kati ya Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na vikundi vya waasi; Nyaraka mbalimbali zitakazoongoza utendaji wa shughuli za Jopo la Pamoja la Mpatanishi wa Umoja wa Afrikana Jopo la Wawezeshaji wa EAC-SADC; pamoja na Mpango wa Utafutaji wa Rasilimali za Kuwezesha Utekelezaji wa Mchakato wa Kurejesha Amani Mashariki mwa DRC.

115. ***Mheshimiwa Spika***, Mwezi Agosti 2025, Wizara iliratibu na kushiriki mkutano wa wataalam kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuhakiki na kukubaliana maandalizi ya Mfumo Jumuishi wa Tahadhari ya Mapema unaozingatia mahitaji ya kila nchi. Lengo la kuandaliwa kwa Mfumo huo ni kuiwezesha Jumuiya kujiandaa na kukabiliana na matishio mbalimbali ikiwemo majanga ya asili, dharura za afya na masuala ya amani, ulinzi na usalama. Mfumo huu uliidhinishwa rasmi mwezi Machi 2026 kupitia Mkutano wa pamoja wa mabaraza ya Ushirikiano katika Ulinzi, Amani na Usalama na Uratibu wa Sera za Mambo ya Nje.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Wizara iliratibu na kuwezesha upatikanaji wa fursa za ufadhili wa wanafunzi watano kusoma shahada ya kwanza katika Chuo Kikuu cha Korea (KDU) kwa fani za kompyuta, akili unde, usimamizi wa hoteli na biashara. Ufadhili huo umewezeshwa kupitia Baraza la Vyuo Vikuu la Jumuiya ya Afrika Mashariki (IUCEA). Aidha, Wizara ilifanikisha upatikanaji wa ufadhili kwa wanafunzi saba wa Tanzania kusoma Shahada ya Uzamili katika masomo ya udaktari, usimamizi wa mazingira, kiswahili, uchumi, na afya ya umma katika vyuo vikuu mbalimbali vilivyopo katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa pamoja wa Mabaraza ya Kisekta ya EAC ya

Uchukuzi, Mawasiliano na Hali ya hewa; Nishati na Madini; na Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji ambapo tathmini ya utekelezaji wa miradi 286 ya miundombinu ilifanyika na miradi mipya 170 ilipendekezwa ikiwemo miradi takriban 45 ya Tanzania inayojumuisha TEHAMA na upanuzi wa reli ya kisasa (SGR) hadi DRC. Miradi hiyo inachangia katika kuimarisha mtangamano wa kikanda, kuendeleza uchumi wa kidijitali na kukuza uwekezaji.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Januari 2026, Wizara iliratibu na kushiriki ziara ya Mheshimiwa, Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ukaguzi wa ujenzi wa Kituo cha Kikanda cha Uratibu wa Uokoaji Majini (MRCC) jijini Mwanza ambacho kitaboresha usalama na utayari wa kukabiliana na matukio ya dharura katika Ziwa Victoria. Kituo hiki cha kikanda kwa sasa kinahusisha nchi mbili ambazo ni Tanzania na Uganda. Aidha, kituo kitaanza kutoa huduma kwa wananchi wa eneo husika mara baada ya kukamilika kwa taratibu za utumishi.

119. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, mwezi Januari 2026, Wizara ilikagua Kituo cha Kutoa Huduma kwa Pamoja Mpakani (OSBP) cha Namanga ili kujiridhisha na utendaji wa huduma za Himaya Moja ya Forodha, kutatua kero za wafanyabiashara na kuongeza uelewa wa fursa za biashara ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pia, Wizara iliratibu na kushiriki ziara ya Kamati ya Mawasiliano, Biashara na Utalii ya Bunge la Afrika Mashariki katika OSBP ya Holili/Taveta kwa lengo la kukagua utendaji na hali ya miundombinu. Kamati hiyo iliridhishwa na utendaji wa Kituo hicho, na kushauri changamoto zilizopo za ukosefu wa mashine ya ukaguzi wa mizigo mikubwa na mifumo ya kuhakiki mizigo kutowiana zitatuliwe ili kurahisisha ufanyaji biashara.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Januari 2026, Wizara iliratibu na kushiriki ziara ya Mheshimiwa Dkt. Ruth Nankabirwa Ssentamu, Waziri wa Nishati na Maendeleo ya Madini wa Uganda, katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) upande wa Tanzania. Ujenzi wa mradi huo umefikia **asilimia 79** na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai 2026. Kukamilika kwa Mradi huo kunatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali, kuimarisha uwekezaji katika sekta ya nishati na fursa za ajira kwa Watanzania.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Mei 2026, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya maandalizi ya Zoezi la 14 la Pamoja la Vituo vya Uamrishaji vya Kijeshi la Jumuiya ya Afrika Mashariki (Ushirikiano Imara 2026), lililofanyika Nairobi, Kenya. Zoezi hilo, lililenga kujenga uwezo wa wataalam wa Nchi Wanachama katika operesheni za ulinzi wa amani, mapambano dhidi ya ugaidi na uharamia pamoja na mbinu za kukabiliana na majanga.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Aprili 2026, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 13 wa Pamoja wa Mabaraza ya Kisekta ya Mawaziri wa Ushirikiano katika Ulinzi, Amani na Usalama na Uratibu wa Sera za Mambo ya Nje uliofanyika Nairobi, Kenya. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mhe. Patrobasi Katambi (Mb), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Mkutano ulijadili masuala mbalimbali yaliyohusu amani, ulinzi na usalama ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Kituo cha Kitaifa cha Tahadhari ya Migogoro na mfumo wa kushughulikia wahamaji wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki waliokwama nje ya jumuiya.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi 2026, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Wakuu wa Viwanda vya Kijeshi uliofanyika Kigali, Rwanda. Mkutano ulipokea na kujadili taarifa za nchi wanachama

kuhusu maendeleo ya matumizi ya vifaa vya ulinzi vya pamoja, utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Kisekta la Ushirikiano katika Ulinzi. Vilevile, mkutano ulitoa fursa kwa nchi wanachama kufanya maonesho ya bidhaa na huduma zitokanazo na viwanda vya kijeshi.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Aprili 2026, Wizara iliratibu na kushiriki katika Kongamano la Nne la Sayansi, Teknolojia na Ubunifu la Jumuiya ya Afrika Mashariki lililofanyika Kigali, Rwanda. Kongamano hilo lililenga kuhamasisha matumizi ya Akili Unde katika kukuza ubunifu na maendeleo jumuishi.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Kongamano hilo, mikakati muhimu ya kikanda ilizinduliwa ikiwemo; Mkakati wa Sayansi ya Anga na ule wa Kuendeleza Viwanda vya Ubunifu katika Teknolojia ya Habari pamoja na mfumo wa kuboresha elimu, ujuzi na ubunifu ili kukuza sekta ya Akili Unde katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, vijana watatu wa Kitanzania walitunukiwa tuzo kutokana na bunifu walizozifanya katika matumizi ya Akili Unde kwenye masuala ya fedha, utengenezaji wa mbolea kutoka masalio ya kilimo na mashine nafuu za kilimo. Pamoja na tuzo hizo, Tanzania imeombwa kuwa mwenyeji wa Kongamano la Tano linalotarajiwa kufanyika mwaka 2028, hatua itakayofungua fursa zaidi kwa wabunifu na wajasiriamali wa ndani.

**Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA)**

126. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu na kufanikisha ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA) ambapo katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bunge hilo lilijadili na kupitisha maazimio mbalimbali ambayo yanaimarisha Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kama ifuatavyo:

(i) Azimio la Bunge Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025;

(ii) Azimio la Bunge kulihimiza Baraza la Mawaziri na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuharakisha mchakato wa kutekeleza mifumo ya Kanda ya Viwanda na ongezeko la thamani ya bidhaa ili kupunguza uuzaji wa malighafi nje ya Jumuiya. Hatua hii, itawezesha matumizi ya rasilimali ghafi ili kuimarisha minyororo ya thamani katika bidhaa zinazozalishwa ndani ya Jumuiya ikiwa ni jitihada za kumudu ushindani katika soko la kimataifa; na

(iii) Azimio la Bunge kulihimiza Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki kuimarisha upatikanaji wa chakula kwa bei nafuu katika Jumuiya. Hatua hii itawezesha Jumuiya kuwa na chakula cha kutosha na kukabiliana athari za mabadiliko ya tabianchi yanayoweza kusababisha uhaba wa chakula.

127. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, katika kipindi hiki, Bunge la Afrika Mashariki lilijadili na kupitisha miswada

mitatu ya sheria ili kuimarisha Ajenda ya Mtangamano wa Kikanda kama ifuatavyo:

(i) Muswada wa Sheria wa Kuanzisha Taasisi ya Takwimu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 2025. Sheria hii inaweka utaratibu wa kuwa na Taasisi ambayo inasimamia kuoanisha takwimu za Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki sanjari na kusimamia utekelezaji wa masuala muhimu ikiwemo vigezo vya muunganiko wa uchumi jumla wa Nchi Wanachama;

(ii) Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 2025. Sheria hii inalenga kurahisisha na kuboresha shughuli za usimamizi wa forodha na taratibu zake ikiwemo, kuondoa kodi katika bidhaa pindi kutakapotokea upungufu katika uzalishaji wa bidhaa katika Jumuiya; na

(iii) Muswada wa Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu uzuiaji wa mtiririko haramu wa fedha. Sheria hii inaweka utaratibu wa pamoja miongoni mwa Nchi Wanachama za Jumuiya kuzuia utokaji haramu wa rasilimali za Jumuiya hususan rasilimali fedha ili kuimarisha uwezo wa kanda wa kukusanya rasilimali za ndani, kuongeza fursa za ajira, na kuvutia wawekezaji.

**Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki**

128. ***Mheshimiwa Spika***, Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACJ) ni chombo cha kutoa haki na kutafsiri Sheria na Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mahakama hii inatekeleza

majukumu yake kama sehemu ya kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya mtangamano wa kikanda.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Tanzania kupitia Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulimteua Mheshimiwa Jaji Diejo Stephen Abraham kutoka Jamhuri ya Sudani Kusini, Jaji Abdiwahid Warsame Abdullahiwa kutoka Shirikisho la Jamhuri ya Somalia na Mhe. Anne Atieno Amadi kutoka Jamhuri ya Kenya kuwa Majaji wa Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kipindi cha kuanzia tarehe 7 Machi, 2026.

## Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

130. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Julai 2025, Tanzania ikiwa Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya SADC, Wizara iliratibu Mkutano wa 27 wa Kamati ya Mawaziri wa Asasi hiyo uliofanyika jijini Dar es Salaam. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo ulijadili na kukubaliana hatua za kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika ulinzi na usalama ikiwemo mapambano dhidi ya uhalifu unaovuka mipaka, rushwa na ugaidi; utatuzi wa migogoro; na kuimarisha demokrasia.




*Mawaziri kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kwenye Mkutano wa 27 wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jumuiya hiyo uliofanyika jijini Dar es Salaam.*

131. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mkutano huo, Tanzania iliendelea kuimarisha ushawishi wake wa kidiplomasia kwa kuongoza majadiliano yaliyofanikisha maamuzi muhimu kuhusu ajenda ya amani, ulinzi na usalama katika Kanda. Utekelezaji wa maamuzi hayo, utachangia kuimarisha hali ya amani na utulivu na kuepusha matishio ya kiusalama na migogoro yenye athari za moja kwa moja kwa Tanzania na Kanda kwa ujumla.

132. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Mkutano huo ulichagiza shughuli za kiuchumi na mapato kwa watoa huduma za malazi, usafiri, chakula, utalii na huduma nyingine za kijamii kutokana na wageni takriban 500 kuingia nchini kuhudhuria Mkutano husika.

133. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Agosti 2025, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 45 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika Antananarivo, Madagascar. Katika Mkutano huo, Tanzania ilifanikiwa kushawishi

SADC kutekeleza maazimio ya Mkutano wa Nishati wa Afrika wa *Mission 300* uliofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Januari 2025. Hatua hii imefungua fursa za upatikanaji wa rasilimali kwa miradi ya nishati hapa nchini na katika ukanda wa SADC. Aidha, Mkutano huo, uliridhia kuunga mkono wagombea sita wa Tanzania katika nafasi mbalimbali za kimataifa, ikiwa ni hatua muhimu ya kuchagiza ushindi wa wagombea wetu.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa nafasi yake ya Mwenyekiti anayemaliza muda wake wa Utatu wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama (*Organ Troika*) Tanzania ilishiriki katika utatuzi wa migogoro ambapo Wizara iliratibu na kushiriki Mikutano ya Dharura ya Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu mgogoro wa kisiasa nchini Madagascar iliyofanyika mwezi Oktoba, Novemba na Desemba 2025. Halikadhalika, mwezi Oktoba 2025 Tanzania ilishiriki kwenye Misheni ya Utambuzi wa Mgogoro (*Fact Finding Mission*) nchini Madagascar. Misheni hiyo iliainisha chanzo, wahusika na madhara ya mgogoro huo na kupendekeza hatua za kuchukuliwa. Ushiriki huu umeendelea kuimarisha uzoefu na nafasi ya Tanzania katika juhudi za usuluhishi na udhibiti wa migogoro katika kanda.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi 2026, Wizara iliratibu na kuongoza ujumbe wa Tanzania ulioshiriki Mkutano wa Baraza la Mawaziri la SADC uliofanyika Pretoria, Afrika Kusini. Pamoja na masuala mengine, Baraza lilijadili na kupitisha Bajeti ya SADC kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ambayo pia ilijumuisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya uhakiki wa nyaraka muhimu za SADC zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, Baraza lilielekeza Sekretarieti ya SADC kuharakisha ukamilishaji wa Makala Jongefu ya Machapisho ya Brigedia Jenerali (Mst.) Hashim Mbita kuhusu historia ya harakati za ukombozi kusini mwa Afrika.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano huo, Tanzania iliwasilisha hoja kuhusu uanzishwaji wa Mfumo wa Kisera, Kisheria na Kitaasisi wa Usimamizi wa Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani (*One Stop Border Posts - OSBP*). Kwa sasa, maandalizi ya Mfumo yanaendelea ndani ya nchi wanachama. Kukamilika kwa Mfumo huo kutarahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma za mipakani na hivyo kuongeza fursa za kibiashara na kiuchumi katika Kanda.

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu ushirikiano wa kibiashara baina ya Tanzania na nchi wanachama wa SADC, hatua iliyochochea ongezeko la mauzo ya nje kutoka **Dola za Marekani milioni 2,968** mwaka 2024 hadi **milioni 3,545** mwaka 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 19.4.** Sambamba na hilo, uagizaji kutoka SADC umeongezeka kutoka **Dola za Marekani milioni 786.4** hadi Dola za Marekani **milioni 837.9** sawa na ongezeko la **asilimia 6.5**. Kutokana na mwenendo huu, Tanzania inaendelea kunufaika na urari chanya wa biashara ndani ya SADC.

**Jumuiya ya Nchi za Mwambao wa Bahari ya Hindi**

138. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Wizara imeendelea kuratibu shughuli za Jumuiya ya Nchi za Mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA) hususan uchumi wa buluu, utunzaji wa mazingira na usalama wa bahari. Mathalan, mwezi Desemba 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mdahalo wa Biashara wa Jumuiya ya IORA uliofanyika Maputo, Msumbiji. Mdahalo huo uliwezesha Wataalam kubadilishana maarifa na uzoefu kuhusu mwenendo wa biashara na uwekezaji katika ukanda wa Bahari ya Hindi na namna ya kunufaika na fursa zilizopo katika Uchumi wa Buluu hususan kwa vijana na wanawake.

139. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika kipindi hiki Wizara iliratibu ushiriki wa Wataalam wa Tanzania katika warsha mbalimbali za kitaalam zilizoandaliwa na Jumuiya ya IORA. Warsha hizo zilijikita katika namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; usimamizi wa rasilimali za maji; kukabiliana na maafa; matumizi ya bahari kuzalisha nishati; usalama na usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari; pamoja na usimamizi wa ikolojia ya bahari.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wataalam walipata fursa ya kubadilishana maarifa na uzoefu na washiriki wengine kuhusu umuhimu wa matumizi ya mbinu asilia katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; matumizi ya teknolojia bunifu ya nishati bahari kama sehemu ya jitihada za kuongeza matumizi ya nishati safi; na ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi na udhibiti wa maafa.

141. ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika, kupitia Warsha hizo, Wataalam wetu walipata fursa ya kujengewa uwezo kuhusu matumizi ya teknolojia bunifu ya kuondoa chumvi kwenye maji ya bahari (*Ocean Water Desalination*) kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya shughuli za kibinadamu. Teknolojia hii mbadala ni muhimu hususan katika kipindi hiki ambapo kumekuwa na ongezeko la uhaba wa maji safi unaochochewa na mabadiliko ya tabianchi; ongezeko la idadi ya watu; na ukuaji wa miji.

142. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi 2026, Wizara iliratibu na kuongoza ujumbe wa Tanzania ulioshiriki katika Maadhimisho ya miaka 29 tangu kuanzishwa kwa IORA. Maadhimisho hayo yalihusisha upandaji miti kama sehemu ya kuunga mkono kampeni ya Kitaifa ya Upandaji miti ya "27 ya Kijani" ikiwa ni maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** maadhimisho hayo ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024 na Nguzo Na. 3 ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kuhusu uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, maadhimisho hayo yalijumuisha mazoezi ya viungo na mbio za taratibu kama sehemu ya kuhamasisha jamii yenye afya bora kupitia Kauli Mbiu ya "*IORA improves lives.*"

**Umoja wa Afrika (AU)**

144. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Februari 2026, Wizara iliratibu ushiriki wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Jijini Addis Ababa, Ethiopia. Mkutano huo uliteua Kamati ya Uongozi ya Umoja wa Afrika kwa mwaka 2026 ambapo Jamhuri ya Burundi iliteuliwa kuwa Mwenyekiti. Nchi nyingine zilizoteuliwa ni Ghana kutoka Kanda ya Magharibi, Makamu wa Kwanza wa Mwenyekiti; Tanzania kutoka Kanda ya Mashariki, Makamu wa Pili wa Mwenyekiti. Vilevile, nchi ya Angola iliteuliwa kuwa Katibu *(Rapporteur)*.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia uteuzi huo, na ushawishi wa Tanzania katika Umoja wa Afrika inatarajiwa kuwa mwaka 2027 Tanzania itakuwa Makamu wa Kwanza wa Mwenyekiti na mwaka 2028 itakuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika.

146. ***Mheshimiwa Spika,*** Mkutano huo pia ulimteua na kumpitisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Kinara wa Umoja wa Afrika katika masuala ya Afya ya Mama na Mtoto (*AU Champion for Maternal and Child Health*).

Kuteuliwa kwa Mheshimiwa Rais ni kielelezo cha kutambua jitihada zake na za Serikali anayoingoza katika kuzuia vifo vya wakinamama na watoto hapa nchini na barani Afrika. Aidha, hatua hii muhimu ni ishara ya Tanzania kuendelea kuaminika kikanda na kimataifa.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, Mkutano uliiteua Tanzania kuwa Mjumbe wa Kudumu wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali Kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (CAHOSCC). Aidha, kufuatia ushawishi wa Tanzania, Umoja wa Afrika ilikubali Tanzania kuwa mwenyeji wa Kituo cha Mafunzo ya Vijana kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Hatua hii muhimu itaiwezesha Tanzania kushiriki kwenye vikao vyote na kutoa mchango wake kuhusu namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Mkutano wa 39 uliidhinisha Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika *(African Liberation Heritage Centre – ALHC)* kilichopo nchini Tanzania kuwa Taasisi Maalum ya Umoja wa Afrika (AU) na kuzisisitiza Nchi Wanachama, Taasisi za Kikanda, na Washirika wa Kimataifa kutambua umuhimu wa Kituo hicho katika kuhifadhi urithi wa ukombozi wa Afrika kwa vizazi vijavyo.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Mheshimiwa *Balozi* Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Mkutano wa Saba wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika na Umoja wa Ulaya (AU – EU), pamoja na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kuhusu Maboresho ya Taasisi za Umoja wa Afrika, iliyofanyika Luanda, Angola. Ushiriki wa Tanzania kwenye Mikutano hiyo umeimarisha ushirikiano na kutoa nafasi kwa Tanzania kuwasilisha msimamo wake kuhusu maeneo ya

kipaumbele kwenye ushirikiano kati ya Afrika na Umoja wa Ulaya.

150. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Agosti 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Jukwaa la Mfumo wa Chakula Barani Afrika (AGRF 2025), lililofanyika nchini Senegal. Kupitia Jukwaa hilo, Tanzania ilitangaza fursa za ushirikiano na uwekezaji zilizopo kwenye sekta ya kilimo na kuonesha hatua zilizochukuliwa katika mageuzi ya mifumo ya kilimo na chakula nchini.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Mawaziri wa Afya kuhusu Uzalishaji wa Dawa Barani Afrika uliofanyika Algiers – Algeria. Katika mkutano huo, Tanzania kupitia Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na Wakala wa Dawa na Vifaa Tiba wa Algeria zilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika uzalishaji na usambazaji wa dawa. Aidha, Bohari ya Dawa (MSD) ilianzisha ushirikiano na kampuni tano za dawa, hatua inayochochea uzalishaji na upatikanaji wa dawa nchini.

**Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR)**

152. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Mheshimiwa *Balozi* Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Jumuiya za Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR) uliofanyika Kinshasa, DRC. Katika Mkutano huo, Tanzania ilishiriki katika majadiliano na kutoa maoni yake kuhusu namna ya kuimarisha amani katika Ukanda wa Maziwa Makuu.

153. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Desemba 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Dharura

wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR) na Nchi Wanachama wa Mkataba wa Amani, Usalama na Ushirikiano (*PSC Framework*) uliofanyika Entebbe, Uganda. Katika Mkutano huo, Tanzania ilishiriki katika majadiliano na kutoa mapendekezo kuhusu hatua za kuchukuliwa ili kurejesha amani Mshariki mwa DRC.

**Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA)**

154. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Septemba 2025, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Kazi wa Nne na Mkutano wa 17 wa Baraza la Mawaziri wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA) uliofanyika jijini Cairo, Misri ambapo Tanzania ilikabidhi uenyekiti wa Baraza kwa Misri. Chini ya Uenyekiti wake Tanzania, iliwezesha kupitishwa kwa Itifaki ya Vijana na Wanawake katika Biashara ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kinara wa uhamasishaji wa wanawake na vijana katika biashara ndani ya Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA).

155. ***Mheshimiwa Spika***, Mkutano huo ulipitisha kanuni za utambuzi wa uasili wa bidhaa katika nguo, mavazi na uundaji wa magari, zikilinda malighafi za ndani huku zikiruhusu uagizaji wa malighafi adimu Afrika. Kupitia kanuni hizo, kampuni 50 za Tanzania zilizokidhi vigezo zilipewa cheti cha utambuzi wa uasili wa bidhaa na kufanya biashara ndani ya Soko Huru la Biashara la Afrika na hivyo kuchangia katika kukuza uchumi kupitia biashara na uwekezaji.

**Ushirikiano wa Kimataifa**

156. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Agosti 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Tatu wa Umoja wa Mataifa wa Nchi zisizo na Mlango wa Bahari (*LLDC3*) uliofanyika Awaza, Turkmenistan. Tanzania ikiwa nchi yenye mlango wa Bahari ilitumia fursa hiyo kusisitiza ushirikiano na nchi zisizo na mlango wa bahari katika kufanikisha huduma za usafirishaji wa mizigo inayopita katika bandari za Tanzania. Aidha, Tanzania itaendelea kutumia nafasi yake ya kimkakati na kijiografia kupitia bandari na miundombinu yake ya usafirishaji ambayo inawezesha nchi zisizo na mlango wa bahari kufikia masoko ya kimataifa. Hatua hiyo inaendelea kuchangia kukuza ushirikiano wa kikanda na maendeleo endelevu.

157. ***Mheshimiwa Spika***, halikadhalika, mwezi Agosti 2025, Wizara kwa kushirikiana na UN-WOMEN iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Saba wa Dunia wa Miji Salama uliofunguliwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi uliofanyika Zanzibar. Mkutano huo ulishirikisha Ma-meya zaidi ya 50 kutoka nchi mbalimbali duniani kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali ikiwemo usalama wa wanawake na wasichana katika miji, kuimarisha usawa wa kijinsia, kupambana na ukatili wa kijinsia, pamoja na ujenzi wa miji salama na jumuishi inayochochea maendeleo endelevu ya jamii.

158. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Septemba 2025, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 60 wa Baraza la Haki za Binadamu uliofanyika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa Geneva, Uswisi. Katika Mkutano huo, Tanzania ilijibu shutuma mbalimbali zilizowasilishwa dhidi yake pamoja na kuwasilisha matamko na misimamo kuhusu haki za binadamu ambazo zilihusisha haki ya maendeleo, haki za watoto na wazee, haki za kufanya kazi na haki za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kitamaduni.

159. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Septemba 2025, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 80 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA 80) jijini New York, Marekani ambapo Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongoza ujumbe wa Tanzania. Kupitia Mkutano huo, Nchi Wanachama zilisisitizwa kuhusu utekelezaji wa Ajenda 2030 ya Maendeleo Endelevu, ushirikiano wa kimataifa, amani na kuheshimu sheria za kimataifa. Pembezoni mwa Mkutano huo, ujumbe wa Tanzania ulifanya mazungumzo na viongozi wa Serikali na Sekta Binafsi kutoka nchi mbalimbali kwa lengo la kuimarisha uwekezaji, biashara na diplomasia ya kimataifa.

160. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Septemba, 2025 Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano Mkuu wa 69 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomu *(IAEA)*, uliofanyika Vienna, Austria. Katika Mkutano huo, Tanzania ilipata fursa ya kutoa tamko na kubainisha dhamira yake ya kutumia nyuklia katika kuzalisha nishati, kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na utayari wa nchi katika kutekeleza sera ya shirika la *IAEA* ya matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia kwa maendeleo endelevu.

161. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Oktoba 2025, Wizara iliratibu na kufanikisha hafla ya Utiaji Saini wa Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uhalifu wa Kimtandao (*Hanoi Convention*). Mkataba huo ulitiwa saini Jijini Hanoi, Vietnam, ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitia saini mkataba huo kuunga mkono juhudi za kimataifa za kupambana na uhalifu wa kimtandao. Hatua hii inaashiria dhamira ya Tanzania katika kuimarisha usalama wa kidijitali, kulinda mifumo ya Serikali na Sekta Binafsi, na kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika kukabiliana na uhalifu wa mtandao unaoathiri biashara na huduma za kijamii.

162. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano Mkuu wa 43 wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) uliofanyika Samarkand, Uzbekistan. Katika Mkutano huo, Kiswahili kilipitishwa rasmi kuwa lugha ya Mkutano Mkuu wa UNESCO kuanzia mwaka 2027, hatua ambayo inathibitisha Kiswahili kuwa nyenzo ya kidiplomasia katika nyanja za kimataifa. Vilevile, Tanzania ilichaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Kimataifa la Usimamizi wa Maeneo ya Hifadhi Hai za UNESCO kwa kipindi cha mwaka 2025 hadi 2029, jambo linaloongeza nafasi ya nchi yetu katika usimamizi na uhifadhi wa urithi wa dunia.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Kikao cha 25 cha Nchi Wanachama wa Mkataba wa 1972 wa kulinda na kuhifadhi urithi wa utamaduni na asili, kilichofanyika kwenye Makao Makuu ya UNESCO jijini Paris, Ufaransa. Katika Kikao hicho Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichaguliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Urithi wa Dunia (*World Heritage Committee*) kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka 2025 hadi 2029.

164. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, Wizara ilishiriki na kufanikisha Mkutano wa Uwekezaji uliofanyika nchini Morocco, ambapo Tanzania iliwasilisha Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) Kipande cha 7 (Uvinza–Malagarasi, km 156). Katika Mkutano huo, wawekezaji wa kimataifa wakiwemo JP Morgan, AIIB, Standard Bank/Stanbic Tanzania na Credit Agricole CIB walionesha nia ya kuunga mkono utekelezaji wa mradi husika kwa kutoa ahadi za awali za ufadhili zenye jumla ya takriban **Dola za Marekani bilioni 1.52**.

165. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Novemba 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano Mkuu wa Shirika la Utalii Duniani la Umoja wa Mataifa uliofanyika

Riyadh, Saudi Arabia. Katika Mkutano huo, Chama cha Waendeshaji Utalii Tanzania (TATO) kilipokea Tuzo ya UN Tourism ya *"Promotion of the Affiliate Membership in Africa,"* ikitambua mchango wake katika kukuza ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi, utalii endelevu, ubunifu na uongozi. TATO ilitajwa miongoni mwa wanachama washirika 11 pekee duniani waliotambuliwa kwa kazi zao bora katika mfumo wa kimataifa wa utalii.

166. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kukuarifu kwamba chini ya uratibu wa Wizara, Tanzania imefanikiwa kupata tuzo kadhaa za kimataifa katika sekta ya utalii mwaka 2025. Nchi yetu ilichaguliwa kuwa *World's Leading Safari Destination 2025* kwenye *World Travel Awards Grand Finals* zilizofanyika Bahrain, ikizishinda nchi nyingine maarufu duniani. Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ilitangazwa kuwa Hifadhi bora zaidi duniani kwa mwaka 2025. Aidha, Tanzania ilitambuliwa kama sehemu bora ya Utalii Barani Afrika kwa Mwaka 2025 katika hafla ya Tuzo za Utalii za Afrika na Bahari ya Hindi iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

167. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Novemba 2025, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Maendeleo ya Mawasiliano ya Dunia (WTDC-25) uliofanyika Baku, Azerbaijan. Kupitia mkutano huo, Tanzania ilishinda nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Kikundi cha Utafiti cha *International Telecommunication Union (ITU–D)*, ambapo Mhandisi Imelda Salum Banali alichaguliwa kuhudumu kwa kipindi cha 2026–2029. Hatua iliyoimarisha taswira, nafasi na mchango wa Tanzania katika mashirika ya kimataifa.

168. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 11 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Tumbaku (WHO FCTC COP11) uliofanyika Geneva,

Uswisi. Katika mkutano huo, Tanzania ilieleza msimamo wake wa kupunguza matumizi ya tumbaku kwa kuzingatia miongozo ya WHO FCTC, huku ikitambua mchango wa zao la tumbaku katika uchumi wa taifa, hususan sekta ya kilimo, ajira, na mapato ya kigeni. Uthibiti wa zao hilo utaendelea kutekelezwa kwa kutoa tahadhari za kiafya, bila katazo la ghafla, ili kulinda kipato cha wakulima na kukuza pato la taifa, hasa katika mikoa ya Tabora na Katavi.

169. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2025, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 30 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP30) uliofanyika Belem, Brazil. Aidha, Tanzania ilitumia fursa hiyo kuwasilisha vipaumbele vyake, jitihada zinazotekelezwa na changamoto inazokabiliana nazo katika mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, ujumbe wa Tanzania ulifanya mikutano ya uwili na taasisi muhimu za kimataifa ikiwemo *Green Climate Fund*, UNEP, UNDP, Benki ya Maendeleo ya Afrika na IFAD, hatua iliyochangia kuimarisha ushirikiano uliopo na kuibua fursa mpya za kifedha na kiufundi kwa maendeleo ya nchi.

170. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Desemba 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Saba wa Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEA-7) uliofanyika jijini Nairobi, Kenya, ambapo ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Hayati William Vangimembe Lukuvi (Mb), aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu. Katika Mkutano huo, Tanzania iliwasilisha mafanikio yake katika utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya mazingira, ikiwemo uhuishaji na ukamilishaji wa Mkakati na Mpango wa Taifa wa Uhifadhi wa Bioanuwai (NBSAP) na kushiriki mijadala kuhusu ulimwengu endelevu, mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa bioanuwai na udhibiti wa uchafuzi

wa mazingira. Ushiriki huo uliwezesha Tanzania kubadilishana uzoefu na Nchi Wanachama wengine katika mikakati ya pamoja ya kukabiliana na changamoto za mazingira duniani.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Januari 2026, Wizara iliratibu hafla ya kukaribisha mwaka mpya wa Kibalozi *(Diplomatic Sherry Party)*. Hafla hiyo ilifanyika kwa mara ya kwanza katika Ikulu ya Chamwino, Dodoma. Katika hafla hiyo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwahutubia Waheshimiwa Mabalozi wanaowakilisha nchi zao nchini pamoja na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa. Katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais alisisitiza umuhimu wa kudumisha ushirikiano baina ya Tanzania na nchi rafiki, Jumuiya za Kikanda na Taasisi za Kimataifa. Aidha, Mheshimiwa Rais, alisisitiza kuwa ushirikiano huo utajielekeza kwenye maeneo yenye manufaa ya kiuchumi, biashara, uwekezaji na maendeleo kwa pande zote mbili badala ya kutegemea misaada. Vilevile, Mheshimiwa Rais alisisitiza kuwa, Tanzania itaendelea kuwa kitovu cha amani, demokrasia, haki za binadamu na utawala bora.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiwa na Waheshimiwa Mabalozi wanaowakilisha nchi zao hapa nchini pamoja na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa kwenye hafla ya kukaribisha mwaka mpya wa Kibalozi (Diplomatic Sherry Party-2026).*

172. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Wizara iliratibu mikutano ya miadi ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mabalozi, na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa waliopo nchini, ambapo masuala mbalimbali ya ushirikiano yalijadiliwa. Hatua hiyo imezidi kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia na kutambulisha fursa za kimkakati zilizopo Zanzibar ikiwemo katika sekta za afya, elimu, utalii, nishati, na uchumi wa buluu kama hatua muhimu katika utekelezaji wa  Sera ya Mambo ya Nje ya Mwakja 2001, Toleo la Mwaka 2024.

173. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Januari 2026, Wizara iliratibu na kushiriki ziara ya kikazi ya ujumbe wa Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), ulioongozwa na Mhe. Eve Bazaiba Masudi, Waziri wa Nchi anayeshughulikia Masuala ya Jamii. Lengo la ziara hiyo lilikuwa kutembelea kambi na kujadili masuala ya wakimbizi  katika kambi ya Nyarugusu, Kigoma. Aidha, ziara hiyo ilibaini uwepo wa changamoto mbalimbali ikiwemo huduma duni za afya, elimu, makazi na nishati ya kupikia  ambazo zinaathiri zaidi watoto na wanawake. Aidha, Tanzania, DRC na UNHCR zilikubaliana kuharakisha utekelezaji wa suluhu ya kudumu, hususan urejeshwaji wa wakimbizi ambao walionesha dhamira ya kurejea kwa hiari nchini mwao.

174. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Februari 2026, Wizara iliratibu ushiriki wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika kuanzia tarehe 3 hadi 5 Februari 2026 Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu. Katika mkutano huo, Mheshimiwa Rais aliwasilisha fursa za uwekezaji zilizopo nchini, akisisitiza sera thabiti, mazingira rafiki ya biashara na umuhimu wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi. Aidha, alishiriki katika majadiliano ya

ngazi ya juu, mikutano ya pande mbili na viongozi mbalimbali pamoja na vikao vya mawaziri vilivyojadili mwelekeo wa maendeleo ya dunia baada ya mwaka 2030, hivyo kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi, biashara na utalii.

175. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Februari 2026, Wizara iliratibu ushiriki wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Kikao cha Kamati ya Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi kilichofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia. Katika kikao hicho, Mheshimiwa Rais alieleza athari za mabadiliko ya tabianchi kwa sekta mbalimbali muhimu nchini na hatua zinazochukuliwa kukabiliana nazo, ikiwemo uwekezaji katika nishati jadidifu na kuimarisha mifumo ya tahadhari ya mapema. Kwa ujumla, viongozi walikubaliana kuipa Afrika nafasi katika uchumi wa kijani, kuboresha upatikanaji wa fedha za tabianchi, kuimarisha usalama wa chakula na kuhakikisha mabadiliko ya nishati yanafanyika kwa usawa.

176. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Februari 2026, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania *(TAEC)* iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Kikanda kuhusu Mpango wa Kuimarisha uwezo wa Nchi Wanachama katika utambuzi na matibabu ya saratani kanda ya Afrika uliofanyika Zanzibar.

177. ***Mheshimiwa Spika***, katika mkutano huo Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alifungua Mkutano huo ambapo alihimiza Nchi Wanachama kuimarisha uwezo wa Taasisi za ndani, ushirikiano wa kikanda na matumizi bora ya sayansi na teknolojia katika kukabiliana na saratani.

178. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia mpango huo, Tanzania inanufaika na upatikanaji wa teknologia, vifaa vya kisasa na mafunzo ya muda mfupi na mrefu na rasilimali watu kupitia ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa. Aidha, Tanzania inatekeleza jumla ya miradi 12 kupitia ushirikiano wa kiufundi na Shirika la Atomiki Duniani (IAEA) kwa lengo la kuimarisha uwezo wa sekta ya afya hususan katika huduma za saratani nchini.

**Utekelezaji wa diplomasia ya Uchumi**

179. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024 hususan diplomasia ya uchumi, Wizara imeratibu upatikanaji wa fursa mbalimbali za kiuchumi kama ilivyoainishwa katika malengo mahsusi ya Sera. Utekelezaji wa diplomasia ya uchumi umejumuisha masuala mahsusi kama vile uwekezaji, fursa za masomo, kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania, utalii, uchumi wa buluu, ajira kwa watanzania na upatikanaji wa mikopo na misaada yenye masharti nafuu. Aidha, utekelezaji wa diplomasia ya uchumi pia ulihusisha masuala yasiyo ya kijadi ikiwemo siasa, ulinzi na usalama kama hatua muhimu na ya kimkakati ili kufikia malengo ya kiuchumi.

180. ***Mheshimiwa Spika***, naomba nilijulishe Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu itaendelea kuwa kiungo na mwezeshaji nambari moja wa masuala muhimu na ya kimkakati ikiwemo ya kisekta hapa nchini. Hatua hii inahusisha upatikanaji wa fursa mbalimbali za kisekta ikiwemo uwekezaji, utalii, misaada na mikopo ya masharti nafuu, ajira za Watanzania nje ya nchi na nafasi za uongozi katika taasisi za kimataifa na upatikaji wa fursa za ufadhili wa masomo kwa vijana.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Septemba 2025, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Jukwaa la Biashara

na Uwekezaji kati ya Tanzania na Marekani, lililofanyika pembezoni mwa Mkutano wa 80 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, jijini New York. Katika Jukwaa hilo, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongoza ujumbe wa wafanyabiashara wa Tanzania kwenye jukwaa hilo.

182. ***Mheshimiwa Spika***, katika Jukwaa hilo, Tanzania ilipata fursa mbalimbali ikiwemo; Mfuko wa Abbort kuthibitisha (affirm) utayari wa mfuko huo kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha Huduma za Upimaji Afya wa Haraka (*Rapid Diagnostic Test -RDTs*) kufikia mwezi Agosti, 2026; Kampuni ya uwekezaji ya Kostiv kuahidi kuongeza uwekezaji wake kwa kujenga hoteli kubwa ya kifahari katika eneo la uhifadhi la Ngorongoro; Kampuni ya Nishati ya USLPG Energy ilitangaza kuanza uwekezaji wa kiasi cha Dola za Marekani Milioni 10 katika sekta ya gesi Afrika ambapo Tanzania itakuwa moja ya nchini itakayo nufaika.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Januari 2026, Wizara iliratibu na kushiriki katika ziara ya kikazi ya Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, jijini London, Uingereza. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kukutana na wafanyabiashara na wawekezaji wa Uingereza na kueleza kuhusu maboresho ya mazingira ya biashara na uwekezaji yanayofanywa na Serikali hapa nchini. Katika ziara hiyo, Mhe. Waziri alikutana na wafanyabiashara na wawekezaji wapatao 150 kupitia majukwaa manne ya Biashara na Uwekezaji yaliyofanyika jijini humo. Miongoni mwa manufaa ya ziara hiyo ilikuwa ni kuongeza imani ya wawekezaji kutoka nchini Uingereza.

184. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile Mhe. Waziri alifanya mazungumzo na taasisi mbalimbali zenye nia ya kuwekeza nchini. Miongoni mwa taasisi hizo ni SinoAm

LLC, ambayo imeonesha nia ya kuwekeza zaidi ya Dola za Marekani Bilioni tano katika sekta ya miundombinu, ikiwemo reli ya kisasa (SGR) katika Ushoroba wa Mtwara, Bandari ya Mtwara na barabara ya Dar - Morogoro Expressway, kupitia mfumo wa ushirikiano wa Sekta Binafsi na Sekta ya Umma (PPP).

185. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na taasisi hiyo, Kampuni ya *Perenco Group* pia ipo katika hatua za mwisho za kuwekeza zaidi ya **Dola za Marekani milioni 300** katika mradi wa uzalishaji umeme kupitia mfumo wa upepo, mkoani Singida. Mradi huu ukikamilika utaongeza Megawati 200 katika gridi ya Taifa ya umeme na kuchangia upatikanaji wa nishati safi nchini.

186. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Oktoba 2025, Wizara iliratibu ziara ya Dkt. Youn Young-MI, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Uingizaji Bidhaa Nchini Korea (*Korea Importers Association* - KOIMA) iliyofanyika hapa nchini. Katika ziara hiyo, ujumbe wa KOIMA ulitembelea na kufanya mazungumzo na kampuni za Mohamed Interprises Tanzania Limited (*MeTL Group*); Uongozi wa Eneo Huru la Uzalishaji Bidhaa kwa ajili ya Masoko ya Nje la Benjamin Mkapa (Benjamin Mkapa -EPZA); Uongozi wa Jukwaa la Kidigitali la Uendeshaji wa Minada ya Bidhaa Tanzania (*Tanzania Mercantile Exchange-TMX*). Wakati wa ziara hiyo, kulifanyika pia kongamano la biashara na uwekezaji kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji nchini na upatikanaji wa masoko kwa bidhaa za Tanzania nchini Korea. Aidha, kongamano hilo lilifungua fursa kwa wadau kubadilishana uzoefu na kujifunza taratibu na masharti ya uingizaji wa bidhaa nchini Korea Kusini.

187. ***Mheshimiwa Spika***, miongoni mwa manufaa yaliyotokana na ziara hiyo ni pamoja na kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano (MoU), kati ya Shirikisho la Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) na Taasisi ya KOIMA, yenye malengo ya kukuza ushirikiano baina ya

taasisi hizo katika kusaidia wafanyabiashara wa Tanzania kuingiza bidhaa katika soko la Korea.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Agosti 2025, niliongoza ujumbe wa Tanzania katika Kongamano la Biashara kati ya Afrika na Singapore lililohusisha wafanyabiashara 15 ambapo Tanzania ilifanikiwa kutangaza fursa za biashara na miradi ya uwekezaji katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi na kuunganisha wafanyabiashara wa Tanzania na Singapore.

189. ***Mheshimiwa Spika***, wakati wa kongamano hilo, Benki ya TCB na Kampuni ya *Robust International Ltd* ya Singapore zilisaini Mkataba wa thamani ya **Dola za Marekani milioni tano** wa kuwezesha usafirishaji wa bidhaa za Tanzania kwenda katika soko la Singapore. Mkataba huo unatarajiwa kuongeza mauzo ya nje na kukuza biashara ya kimataifa pamoja na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Februari 2026, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya pamoja iliyohusisha Waheshimiwa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Zambia katika Kituo cha kutoa Huduma kwa Pamoja Mpakani (OSBP) cha Tunduma/Nakonde. Wakati wa Ziara hiyo, Mawaziri hao walikagua Kituo hicho na baadae kujadiliana namna ya kupatia ufumbuzi changamoto za kiuendeshaji, kimfumo na kimiundombinu zinazokikabili Kituo hicho.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia ziara hii, tuliweza kukwamua vikwazo vitano vya kibiashara ambavyo ni; Uendeshaji kamili wa saa 24 wa Kituo badala ya saa 12 ilivyo sasa kwa upande wa Zambia; Zambia kukamilisha ujenzi wa eneo la kuegesha malori ya mizigo upande wa Zambia yanayosubiri taratibu za kiforodha; Kukamilisha uunganishwaji wa mifumo ya kieletroniki ya kurahisisha taratibu za usafirishaji za bandari (*Integration of Tanzania*

*Electronic Single Window System* (TESWS) *into the TPA's Terminal Operating System* (TOS); Uwasilishaji wa *Mobile Scanner* iliyotolewa na Serikali ya Tanzania kwa Serikali ya Zambia; na Tanzania kukamilisha upanuzi wa barabara ya mchepuo ndani ya kipindi cha miezi sita; na upande wa Zambia kukamilisha miundombinu ya forodha kabla ya mwezi Juni 2026.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Oktoba 2025, Wizara ilishiriki Mkutano wa tisa wa Tume ya Pamoja ya Biashara kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kenya *(9th JTC)* uliofanyika jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulijadili jumla ya vikwazo vya biashara visivyo vya kiforodha 14 vikiwemo vikwazo sita kwa upande wa Tanzania na vinane kwa upande wa Kenya. Vikwazo vinne kati 14 vilipatiwa ufumbuzi. Aidha, vikwazo vingine kumi vipo katika hatua mbalimbali za kupatiwa ufumbuzi.

**Ziara za Viongozi wa Kitaifa Nje ya Nchi**

193. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza dhana ya diplomasia ya uchumi, Wizara imeratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika maeneo ya kimkakati nje ya nchi. Ushiriki wa viongozi katika ziara hizo ni sehemu ya kutafuta fursa za kiuchumi na kuimarisha ushirikiano uliopo baina ya Tanzania na mataifa hayo na mashirika ya kikanda na kimataifa. Naomba nizitaje ziara za Viongozi Wakuu wa kitaifa zilizofanyika katika kipindi hiki kama ifuatavyo:

(i) Ziara ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kushiriki Mkutano wa Pili wa Uvumbuzi wa Nishati ya Nyuklia Barani Afrika, mwezi Mei 2026, Kigali, Rwanda;

(ii) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kushiriki Sherehe za Uapisho wa Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda, mwezi Mei 2026;

(iii) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kushiriki Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika mwezi Februari 2026 Addis Ababa, Ethiopia;

(iv) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika mwezi Februari, 2026 Umoja wa Falme za Kiarabu;

(v) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Comoro Julai, 2025 kuhudhuria Maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa nchi hiyo;

(vi) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kushiriki uzinduzi wa *Global Africa Investment Summit* uliofanyika sambamba na mkutano wa Dunia wa Serikali (*World Governments Summit)* mwezi Februari 2026, UAE;

(vii) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika mwezi Februari, 2026 Addis Ababa Ethiopia;

(viii) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Maziwa Makuu mwezi Novemba 2025 nchini Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo;

(ix) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa ukarabati wa miundombinu ya Reli ya TAZARA iliyofanyika mwezi Novemba 2025 nchini Zambia;

(x) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika na Umoja wa Ulaya iliyofanyika mwezi Novemba 2025 nchini Angola;

(xi) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki Mkutano wa 7 wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira (UNEP) na Siku ya Uhuru wa Jamhuri ya Kenya iliyofanyika mwezi Desemba 2025 nchini Kenya;

(xii) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa *Balozi* Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki katika Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi kuhusu hali ya siasa nchini Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo uliofanyika mwezi Desemba 2025 nchini Uganda;

(xiii) Ziara ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa *Africa Forward: Africa – France Partnership for Innovation and Growth Summit* mwezi Mei 2026 Nairobi, Kenya;

(xiv) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki katika Mkutano wa Nne wa Ufadhili kwa Maendeleo uliyofanyika mwezi Julai 2025 nchini Hispania;

(xv) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika iliyofanyika Agosti, 2025 nchini Madagascar;

(xvi) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki Mkutano wa Pili wa Mazingira Afrika (ACS2) iliyofanyika mwezi Septemba 2025 nchini Ethiopia;

(xvii) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki Mkutano wa 80 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA 80) iliyofanyika mwezi Septemba 2025 nchini Marekani;

(xviii) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki mkutano wa biashara kati ya Afrika na Caribbean kuanzia tarehe 26 Julai hadi 3 Agosti, 2025 iliyofanyika nchini Grenada;

(xix) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Agosti 2025 nchini Burundi katika uzinduzi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kati ya Uvinza na Musongati;

(xx) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika sherehe za uapisho wa Rais Mteule wa Jamhuri ya Malawi mwezi Oktoba 2025 nchini Malawi;

(xxi) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki sherehe ya uapisho wa Rais wa Jamhuri ya Shelisheli tarehe 26 mwezi Oktoba 2025; na

(xxii) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), aliyekuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kushiriki Mkutano wa Mawaziri wa Nishati na Maji

uliofanyika mwezi Julai 2025 nchini Zimbabwe.

### Ziara za Viongozi wa Kitaifa na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa kutoka Nje ya Nchi

194. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Wizara pia iliratibu ziara za kikazi na kitaifa za viongozi wakuu kutoka mataifa mengine nchini kama ifuatavyo:

(i) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda mwezi Februari 2026;

(ii) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa John Dramani Mahama, Rais wa Jamhuri ya Ghana mwezi Machi 2026;

(iii) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda nchini aliyofanya mwezi Mei 2026;

(iv) Ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Dkt. William Samoei Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya aliyofanya mwezi Mei 2026;

(v) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Lazarus McCarthy Chakwera, Rais wa Mstaafu wa Jamhuri ya Malawi na Mjumbe Maalumu wa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, aliyofanya mwezi Aprili 2026;

(vi) Ziara ya Kikazi ya Bi. Mary Porter Peschka, Mkurugenzi wa Shirika la Kimataifa la Fedha Kanda ya Afrika Mashariki, aliyofanya mwezi Aprili 2026;

(vii) Ziara ya Kikazi ya Bw. Christian F. Saunders, Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anayehusika na Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kijinsia aliyofanya mwezi Agosti 2025;

(viii) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Jean-Claude Gakosso, Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Kongo ambaye pia alikuwa Mjumbe Maalumu wa Mheshimiwa Denis Sassou Nguesso, Rais wa Jamhuri ya Kongo aliyofanya mwezi Julai 2025;

(ix) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Kanali Mstaafu Kembo Campbell Mohadi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe mwezi Agosti 2025;

(x) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Filipe Jacinto Nyusi, Rais mstaafu wa Jamhuri ya Msumbiji mwezi Julai 2025; na

(xi) Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Wang Yi, Mjumbe wa Kamati ya Maamuzi ya Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti na Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Watu wa China mwezi Januari 2026.

195. ***Mheshimiwa Spika,*** ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nje ya nchi na Viongozi Wakuu kutoka Mataifa mengine pamoja na wawakilishi wa taasisi za kikanda na kimataifa hapa nchini ni kielelezo cha kukubalika kwa sera na mipango ya Serikali. Aidha, kupitia ziara hizo Serikali imefanikisha upatikanaji wa fursa kupitia mikataba na hati za makubaliano zilizosainiwa na kuimarisha ushirikiano uliopo baina ya pande mbili.

**Masuala ya Itifaki, Uwakilishi na Huduma za Kikonseli**

196. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Wizara iliratibu na kufanikisha utoaji wa huduma za kikonseli na kiitifaki kwa jamii ya wanadiplomasia hapa nchini.

Utekelezaji wa majukumu hayo ni kwa mujibu wa Mkataba wa Vienna kuhusu Uhusiano wa Kidiplomasia wa mwaka 1961 na Mkataba wa Vienna kuhusu Uhusiano wa Kikonseli wa mwaka 1963.

197. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hiki, Wizara ilifanya Mikutano na Mashauriano na Mabalozi na Wakuu wa Mashirika ya Kikanda na Kimataifa hapa nchini. Kupitia mikutano na mashauriano hayo, Wizara ilipata fursa ya kujadili masuala mbalimbali ya ushirikiano baina ya Tanzania na nchi hizo, mashirika ya kikanda na kimataifa.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, Wizara iliratibu na kufanikisha uwasilishaji wa Hati za Utambulisho za Waheshimiwa Mabalozi Wateule wanaowakilisha nchi zao hapa nchini ambapo mabalozi wa Sudan, Algeria, Uhispania, Angola, Uholanzi, Iran, Slovakia, Namibia, Palestina, Kenya, Serbia, Cote d' Ivoire, Siera Leone, Israel, Belarus na Ghana waliwasilisha Hati za Utambulisho kwa Mheshimiwa Rais.

199. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara yangu, ilifanikisha mpango wa kuwarejesha Watanzania waliokwama Mashariki ya Kati kufuatia mgogoro baina ya Marekani na mshirika wake Israel dhidi ya Iran. Mathalan, hivi karibuni Serikali imefanikiwa kuwarejesha Watanzania waliokuwa wamekwama katika maeneo mbalimbali ya ukanda wa Mashariki ya Kati wakiwemo waliokuwa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Iran.

200. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kujulisha kuwa Wizara inaendelea kushirikiana na Balozi zetu zilizopo eneo la Mashariki ya Kati kufuatilia hali inayoendelea katika Ukanda huo huku msisitizo mkubwa ukiwa ni kuhakikisha usalama wa Watanzania wanaoendelea kusalia katika maeneo hayo.

201. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kulijulisha Bunge lako kuwa, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine ndani ya Serikali, imekamilisha na kukabidhi Hati za Viwanja kwa Balozi na Mashirika ya Kimataifa yenye uwakilishi hapa nchini katika eneo la Kibalozi kwenye Mji wa Serikali Mtumba.

202. ***Mheshimiwa Spika***, ufanikishaji wa zoezi hilo ni hatua muhimu ya kuziwezesha Balozi na Mashirika hayo kuanza taratibu za kuendeleza viwanja hivyo kwa ajili ya ofisi na makazi ya watumishi wao.

203. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia Bunge hili, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Mabalozi na Wakuu wa Mashirika ya Kikanda na Kimataifa hapa nchini utayari wa Serikali kuendelea kufanikisha taratibu zitakazo wawezesha kuendeleza milki hizo na kuhamishia shughuli zao Makao Makuu ya Serikali jijini Dodoma. Aidha, nachukua nafasi hii kuupongeza Ubalozi wa Uganda nchini kwa kuanza kuendeleza kiwanja chao kwa kujenga jengo la Ofisi kwa ajili ya Ubalozi huo.

**Uratibu wa Masuala ya Diaspora**

204. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua mchango wa diaspora katika maendeleo ya Taifa, Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024 imesisitiza umuhimu wa ushiriki na ushirikishwaji kikamilifu wa diaspora katika maendeleo ya Taifa.

205. ***Mheshimiwa Spika,*** diaspora wameendelea kuchangia katika ujenzi wa Taifa lao la asili kwa namna mbalimbali ikiwemo kupitia utumwaji wa fedha nyumbani. Katika kipindi cha mwaka 2024-2025 diaspora wa Tanzania walituma jumla ya **shilingi trilioni 3.313** ikilinganishwa na kiasi cha **trilioni 2.11** kwa mwaka 2023-2024, sawa na ongezeko la **asilimia 57**. Hatua hii

inaakisi umuhimu wa mchango wa diaspora katika maendeleo ya Taifa ikiwemo kuboresha maisha ya familia zao hapa nyumbani, kuongeza uwekezaji na kuchangia ukuaji wa sekta ya fedha nchini. Mwelekeo huu unaakisi imani ya diaspora kwa Sera na mazingira wezeshi yaliyowekwa na Serikali.

206. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Wizara iliratibu na kushiriki katika Kliniki za Huduma kwa Pamoja kwa Diaspora katika nchi za Uholanzi, Ujerumani, Ubelgiji, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Oman na Botswana. Kliniki hizo, zilitumika kuainisha fursa zilizopo nchini, kutoa ufafanuzi wa masuala ya kisera, kutoa huduma mbalimbali kama vile za uhamiaji, Vitambulisho vya Taifa, uwekezaji na huduma za kifedha.

207. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara ilifanya maboresho ya mfumo wa kielektroniki wa usajili wa diaspora kidijitali unaojulikana kama *Diaspora Digital Hub* (DDH), kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa takwimu bora za diaspora ili kuwezesha maamuzi sahihi ya kisera. Maboresho hayo, yalijumuisha kuondoa vipengele visivyo vya lazima na vyenye utata katika mfumo huo. Aidha, hadi tarehe 14 Mei, 2026 jumla ya diaspora wapatao 3,065 wamejisajili katika mfumo huo. Maboresho yaliyofanyika yanategemewa kuongeza idadi ya usajili wa diaspora kupitia mfumo huo.

208. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kushawishi Taasisi za kifedha hapa nchini kuanzisha huduma mahsusi kwa diaspora kama hatua ya kuchochea ushiriki wao katika maendeleo ya Taifa. Huduma hizo ni pamoja na *akaunti ya TCB Nyumbani* kutoka Benki ya TCB; Akaunti ya *Asili* kutoka Benki ya Azania; *Twiga Diaspora Banking* kutoka Benki ya NBC; *Akaunti ya Tanzanite* kutoka Benki ya CRDB; *Akaunti ya Mzawa* kutoka Benki ya Absa na Akaunti ya *NMB-Kwetu* kutoka Benki ya NMB.

209. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia huduma hizi za kiupendeleo, diaspora wamerahisishiwa taratibu za uwekezaji, kutunza na kutuma fedha nyumbani. Kuongezeka kwa huduma hizi, kumeashiria ukuaji wa ushiriki wa diaspora katika uchumi wa Taifa na hivyo kuakisi matakwa ya *Dira 2050* hususan mchango wa sekta binafsi katika uchumi wa Taifa na Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024.

210. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeshawishi diaspora kuwa mstari wa mbele kuwekeza katika sekta mbalimbali ikiwemo miradi ya maendeleo. Mathalan, hadi kufikia mwezi Februari 2026, diaspora wamewekeza katika Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja wa UTT-AMIS kiasi cha **shilingi 11,712,000,000** ikilinganishwa na **shilingi 7,500,000,000** zilizowekezwa Februari 2025. Ongezeko hilo la takribani **asilimia 56**, limechangiwa na juhudi za Wizara kushawishi diapora kuchangia maendeleo ya Taifa lao kupitia uwekezaji.

211. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, Wizara imeendelea kushawishi diaspora kuwekeza katika sekta ya nyumba kwa kununua nyumba na viwanja kupitia Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na kampuni nyingine zinazojihusisha na biashara hiyo, hivyo kuchangia maendeleo ya sekta ya ujenzi na kuongeza upatikanaji wa makazi bora nchini. Mathalan, kwa mwaka huu wa fedha 2025/2026, diaspora wamenunua nyumba zenye thamani ya **shilingi 4,193,249,398**.

212. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuongeza ushiriki wa diaspora wetu kwenye ujenzi wa Taifa, Wizara imekamilisha maandalizi ya utambuzi wa mtawanyiko wa Diaspora ya Tanzania Duniani (*Diaspora Mapping*). Zoezi hili linatarajiwa kufanyika kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia Juni 2026. Aidha, Wizara iko katika mashauriano na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na

Uhamaji (IOM) ili kuwezesha utekelezaji wa jukumu hili muhimu.

**Utoaji Elimu na Taarifa kwa Umma**

213. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na juhudi za kuimarisha upatikanaji wa habari kwa wananchi na wadau mahsusi kuhusu utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024, hususan diplomasia ya uchumi. Katika kutekeleza hilo, Wizara imeongeza matumizi ya mitandao ya kijamii sambamba na njia nyingine za mawasiliano katika kuwajulisha wadau fursa zitokanazo na ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa. Aidha, katika juhudi hizo Wizara imetoa mafunzo kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya Serikali ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mabunge na vyama vya kibunge vya kikanda na kimataifa.

214. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara imeendelea kushirikiana na vyombo vya habari vya ndani na vya kimataifa ikiwemo radio, runinga, magazeti na mitandao ya kijamii ili kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Wizara na Serikali kwa ujumla, mafanikio na ufafanuzi wa masuala mbalimbali. Hatua hii imewezesha Watanzania na Raia wa mataifa mengine kupata taarifa sahihi za masuala yanayoendelea nchini kupitia mikutano na vyombo vya habari, makala na vipindi vya mahojiano vinavyowashirikisha viongozi wa Wizara pamoja na Mabalozi wetu nje ya nchi. Juhudi hizi zimelenga kuelimisha wadau na kulinda taswira na heshima ya Taifa letu katika nyanja ya kimataifa.

215. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia inaendelea na utaratibu wa kutoa machapisho ya Jarida la Wizara

(*Foreign Affairs Bulletin*) linalochapishwa kila robo mwaka. Jarida hilo, ni nyenzo muhimu ya kutoa taarifa za shughuli za Wizara na Serikali kwa umma na kwa Jumuiya ya Wanadiplomasia ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara imeendelea kuandaa na kuchapisha vitabu vya ziara za kimkakati za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vinavyoeleza kwa kina malengo na manufaa ya ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa kupitia ziara tajwa. Aidha, Wizara imeanza kuandaa kitabu kuhusu miaka 65 ya historia ya diplomasia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kitabu hihco kitakuwa na kumbukumbu nzuri kwa ajili ya kuelimisha jamii na jumuiya ya kimataifa kwa ujumla kuhusu historia hiyo.

**Uratibu na Kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara**

216. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Serikali iliajiri Mshauri Elekezi kwa ajili ya kufanya tathmini na kushauri namna bora ya kuendeleza na kusimamia milki za Serikali nje ya nchi. Kufuatia ushauri wa Mshauri Elekezi, Wizara imeandaa na kuanza kutekeleza Mpango wa Serikali wa Miaka Mitano (5) wa Ukarabati na Uendelezaji wa Milki za Serikali Nje ya Nchi kuanzia Robo ya Tatu ya Mwaka wa Fedha 2025/2026. Utekelezaji wa Mpango huo unashirikisha wadau wote muhimu katika Sekta ya umma na Sekta binafsi kuanzia ngazi ya maandalizi hadi utekelezaji wa miradi hiyo.

217. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mpango huo unahusisha matumizi ya vyanzo mbadala vya fedha ikiwemo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Taasisi za Fedha na Sekta Binafsi kwa kuzingatia ufinyu wa bajeti kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Baadhi ya miradi inayotekelezwa

kwa vyanzo mbadala vya fedha ni Ujenzi wa Majengo Pacha ya Vitega Uchumi katika Ubalozi wa Tanzania Nairobi, Kenya na Ujenzi wa Jengo la Kitega Uchumi Kinshasa, DRC kwa ubia na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

218. ***Mheshimiwa Spika***, miradi mingine iliyo katika hatua za majadiliano baina ya Serikali na Benki ya CRDB inajumuisha uendelezaji wa milki katika Balozi za Tanzania Lusaka, Zambia na Bujumbura, Burundi. Aidha, maandalizi ya hatua za awali zinajumuisha maandalizi ya nyaraka za mradi, usanifu, ununuzi wa wakandarasi kabla ya mradi kuanza kutekelezwa. Mathalan, Wizara imeanza maandalizi ya nyaraka na taratibu za awali kwa ajili ya miradi ya Abuja, Nigeria; Kinshasa, DRC; na Addis Ababa, Ethiopia kwa ajili ya kuanza utekelezaji wake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Bado tunawaalika wadau wengine, Benki na Sekta Binafsi pamoja na wawekezaji kujumuika nasi katika fursa hizi kupitia jukwaa hili na kuonana na Mtendaji Mkuu wa Wizara, Katibu Mkuu.

**Utawala na Maendeleo ya Watumishi**

219. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imeajiri jumla ya watumishi 25 ambapo watumishi 15 ni Maafisa Mambo ya Nje Daraja la II, watatu Kada ya Wasaidizi wa Kumbukumbu, wawili Kada ya Katibu Mahsusi, wawili kada ya Afisa Habari, mmoja Afisa Rasilimali watu, mmoja Fundi Sanifu Ujenzi na mmoja Afisa Biashara. Hatua hii imewezesha Wizara kuwa na jumla ya watumishi 748 kati ya 758 sawa na **asilimia 98.7** ya ikama ya Wizara. Watumishi 205 kati ya hao wapo kwenye Balozi za Tanzania nje ya nchi; watumishi 25 wapo katika Ofisi za Mambo ya Nje

Zanzibar, watumishi 34 wapo katika Ofisi ndogo ya Dar es Salaam na 484 wapo Makao Makuu ya Wizara, Dodoma.

220. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa Mabalozi 13. Mabalozi 12 kati ya hao wamepangiwa vituo au kuhamishiwa katika Balozi za Tanzania Beijing, Havana, Lusaka, Moroni, New York, Riyadh, Muscat, Stockholm, Paris, Algiers, Tokyo na Seoul. Aidha, Wizara katika kutekeleza Muundo wake imejaza nafasi za Mkaguzi Mkuu wa Ndani; Mkurugenzi wa Ofisi ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki Zanzibar na Wakurugenzi Wasaidizi watano.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi akitoa maelekezo kwa mabalozi walioteuliwa kuiwakilisha Tanzania katika mataifa mbalimbali.*

221. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, jumla ya Watumishi 48 wa kada mbalimbali waliopo Makao Makuu na katika

Balozi za Tanzania nje walipandishwa vyeo. Watumishi watatu walibadilishwa kada baada ya kukidhi vigezo na uwepo wa nafasi. Aidha, watumishi 89 walithibitishwa kazini.

222. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mafunzo, jumla ya watumishi 170 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi. Watumishi 18 kati ya hao walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na 152 ya muda mfupi. Mafunzo hayo yamewaongezea ujuzi katika maeneo ya diplomasia, lugha, sheria za kimataifa, fedha na uwekezaji, maadili ya utumishi wa umma na uandishi wa nyaraka mbalimbali.

223. ***Mheshimiwa Spika*** katika kipindi hiki, Wizara ilitekeleza urejeshaji wa watumishi 38 kutoka vituo 35 waliomaliza muda wa kuhudumu vituoni kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi Nje. Aidha, jumla ya watumishi 41 wamepelekwa vituoni ili kujaza nafasi zilizokuwa wazi baada ya kukidhi vigezo.

224. ***Mheshimiwa Spika***, aidha, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi wa Makao Makuu na Balozini ikiwemo kununua vitendea kazi kama vile ngamizi, samani za ofisi, mashine za kudurufu nyaraka, kusimika mashine ya upekuzi katika jengo la ofisi ndogo la Wizara jijini Dar es Salaam pamoja na ununuzi wa magari na ukarabati wa ofisi na nyumba za makazi balozini. Vilevile, Serikali imeanza taratibu za ujenzi wa jengo la kisasa la Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nje eneo la Kisakasaka, Zanzibar.

**Usimamizi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara**

225. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara imeendelea kusimamia taasisi zilizo chini yake kwa lengo la kuhakikisha zinafikia malengo ya kuanzishwa kwake. Katika kipindi hiki, taasisi hizo zilitekeleza majukumu kama ifuatavyo:

**Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC*)***

226. ***Mheshimiwa Spika,*** AICC ina jukumu la kuendesha biashara ya mikutano kitaifa, kikanda na kimataifa; upangishaji wa nyumba na ofisi kwa taasisi na watu binafsi; na kutoa huduma za afya kupitia hospitali yake. Aidha, Kituo hiki kinaendesha kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), kilichopo jijini Dar es Salaam.

227. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kituo kilipanga kukusanya kiasi cha **shilingi 33,188,520,841** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato vya ndani. Mapato hayo yatatumika kugharamia uendeshaji wa shughuli za Kituo, mishahara, ununuzi wa vifaa tiba, mikutano na miradi ya maendeleo.

228. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 Kituo kilikusanya kiasi cha **shilingi 18,220,348,739** sawa na **asilimia 55** ya malengo yake ya mwaka. Aidha, katika kipindi hiki, Kituo kilitumia kiasi cha **shilingi 17,701,145,684** sawa na **asilimia 53** ya makadirio ya mwaka.

229. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi hicho, Kituo kilifanikiwa kuhudumia jumla ya mikutano 175 ikiwa mikutano 170 ya kitaifa na 5 ya kimataifa, ambayo ilileta jumla ya washiriki 100,612. Aidha, Kituo kilitoa huduma za matibabu kupitia hospitali yake ambapo wagonjwa

wapatao 79,481 walihudumiwa. Aidha, Kituo kimeendelea kuimarisha huduma katika hospitali yake kwa kuongeza huduma za Kibingwa kutoka 11 katika mwaka wa fedha 2024/2025 na kufikia 12 katika kipindi kilichoishia mwezi Aprili, 2026. Kituo pia kimefanikiwa kununua na kusimika mitambo ya kisasa ya kitabibu ikiwa ni pamoja na *Endosycopic na Ultra Sound Machine.*

230. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Desemba, 2025, Kituo kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kilisaini mkataba na Mkandarasi *M/s China Railway Construction Engineering Group (CRCEG)* kwa ajili ya Ujenzi wa mradi wa kituo kipya cha kisasa cha mikutano cha *Mount Kilimanjaro International Convention Centre* (MK - ICC). Aidha, katika kipindi hicho Mkandarasi alikabidhiwa rasmi eneo la Mradi kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mradi huo.

231. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu wa kimkakati utakuwa na uwezo wa kuhudumia washiriki 5,000 kwenye ukumbi mkuu (*Plenary Hall*) kwa mara moja, kumbi ndogo ndogo (*break-out rooms*) zenye uwezo wa kuhudumia washiriki kuanzia 30 hadi 500, pamoja na ukumbi wenye hadhi ya Rais (*Presidential suite*) unaoweza kuhudumia watu 300 kwa wakati mmoja, ukumbi wa maonesho (*Exhibition Centre*) wenye mita za mraba 20,000 na uwezo wa kuhudumia washiriki wapatao 10,000 kwa wakati mmoja.

232. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, mradi huu unajumuisha Jengo la Utawala lenye mita za mraba 2,600, eneo la maegesho ya magari lenye uwezo wa kuegesha magari 2,000 kwa wakati mmoja, Hoteli ya Nyota Tano yenye vyumba 500 ikiwa ni pamoja na vyumba 15 vyenye hadhi ya watu mashuhuri (*VIPs*), na kazi za nje katika eneo la mradi lenye ukubwa wa mita za mraba 50,000.

233. ***Mheshimiwa Spika,*** awamu ya kwanza ya Ujenzi wa MK - ICC katika eneo la Kijenge-Jijini Arusha inatazamiwa kukamilika ndani ya miezi kumi na nane (18) kuanzia tarehe aliyokabidhiwa mkandarasi eneo la ujenzi. Aidha, kwa kuzingatia ukubwa wa mradi huu, gharama za uwekezaji na mahitaji maalumu ya hotel za Nyota Tano, mradi umegawanywa katika awamu mbili, awamu ya kwanza ikihusisha mambo mengine yote isipokuwa, ujenzi wa hotel ambayo itajengwa katika awamu ya pili.

234. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatazamiwa kuwa chachu kubwa ya shughuli za kiuchumi Jijini Arusha na Taifa kwa ujumla na itaongeza uwezo wa Kituo na Taifa kushindana na Mataifa mengine yenye kumbi kubwa na za kisasa Barani Afrika. Awamu ya kwanza ya mradi huu itagharimu **shilingi 338,068,796,610.17** bila kodi ya ongezeko la thamani.

235. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Kituo kiliboresha huduma za hospitali yake iliyoko mjini Arusha kwa kununua vifaa tiba vya kisasa na kuongeza huduma za kibingwa zinazotolewa kwa wagonjwa. Kwa upande mwingine, Kituo kiliboresha kumbi na ofisi zilizoko Jijini Arusha na Dar es Salaam kwa kufanya ukarabati mkubwa, kufanya maboresho ya mazingira na kununua vifaa vya ukalimani wa lugha za kigeni. Hatua hii imeongeza ufanisi katika kutoa huduma bora za Mikutano na kupelekea Kituo kutunukiwa cheti cha ubora cha Kimataifa (ISO 2015:9001).

236. ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika, baada ya kupokea maelekezo kutoka Serikalini, Kituo kimeanza maandalizi kwa ajili ya kutekeleza mpango wa kujenga ukumbi mkubwa wa mikutano katika jiji la Dodoma. Uwepo wa ukumbi huo utachochea ukuaji wa uchumi wa Jiji la Dodoma, kuongeza fursa za ajira, kuvutia wawekezaji, kuimarisha utalii wa mikutano pamoja na kuimarisha hadhi ya Dodoma kama kitovu cha

diplomasia, biashara na uwekezaji nchini. Aidha, ukumbi huo unatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2030.

## Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Utawala Bora (APRM)

237. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Utawala Bora (APRM) ni wakala maalumu wa Umoja wa Afrika ulioanzishwa mwaka 2003. Malengo ya APRM ni kukuza dhana ya Utawala Bora kwa kutekeleza Sera, Viwango na Taratibu zitakazopelekea kuimarika kwa hali ya kisiasa, kuharakisha kasi ya ukuaji wa uchumi, uhakika wa maendeleo endelevu na kuharakisha mtangamano wa Kikanda na Bara zima la Afrika. Pamoja na mambo mengine, Taasisi ya APRM hufanya tathmini zinazoainisha maeneo ambayo nchi imefanya vizuri ili kuyaendeleza na maeneo yenye changamoto zilizopo ili kuzipatia ufumbuzi.

238. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/2026, APRM Tanzania iliidhinishiwa bajeti ya **shilingi 1,257,428,928**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 567,871,929** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 689,556,999** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha zote ni ruzuku kutoka Serikali Kuu. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili 2026, APRM Tanzania imepokea **shilingi 639,446,510.18** sawa na **asilimia 50.85** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kati ya fedha hizo, **shilingi 377,334,321.03** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 262,112,189.15** ni kwa ajili ya mishahara.

239. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2026, APRM Tanzania imetumia **shilingi 632,369,505.26** sawa na **asilimia 98.89** ya fedha zilizopokelewa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 262,112,189.15** ni kwa ajili ya mishahara

na **shilingi 370,257,316.11** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

240. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 APRM Tanzania imetekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo kuratibu na kufanikisha ziara ya kikazi ya ujumbe kutoka Sekretarieti ya APRM Bara unaoshughulikia masuala ya kuangalia uwezo wa nchi kukopesheka iliyofanyika mwezi Agosti, 2025 hapa nchini. Baadhi ya matokeo muhimu ya ziara hiyo ni kuandaliwa kwa Ripoti ya Ujumbe wa Msaada wa Kiufundi kuhusu Tathmini ya Kimataifa ya Uwezo wa Nchi Kukopesheka ambayo imebainisha changamoto, fursa pamoja na mapendekezo ya kuboresha nafasi ya Tanzania katika tathmini za kimataifa za uwezo wa kukopesheka.

241. ***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti hiyo ni nyenzo muhimu kwa Serikali kwani itasaidia katika kuimarisha maandalizi na uratibu wa Taasisi za Serikali wakati zinapokutana na taasisi ama mashirika ya kimataifa yanayofanya tathmini ya uwezo wa nchi kukopesheka. Aidha, mapendekezo yaliyotolewa yatasaidia kuboresha uwazi wa taarifa za kiuchumi, kuimarisha sera na mifumo ya usimamizi wa uchumi, pamoja na kuongeza uelewa wa wadau kuhusu vigezo vinavyotumika katika tathmini hizo, hali ambayo inaweza kuchangia kuboresha taswira na uaminifu wa Tanzania katika masoko ya fedha ya Kimataifa.

242. ***Mheshimiwa Spika,*** APRM Tanzania ilishiriki katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyofanyika mwezi Julai 2025 pamoja na Maonesho ya 12 ya Kimataifa ya Biashara Zanzibar yaliyofanyika mwezi Januari 2026. Kupitia Maonesho hayo, APRM ilitumia fursa hiyo kuelimisha umma kuhusu dhana ya Utawala Bora na Mpango wa APRM ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa mawasiliano kwa wadau.

243. ***Mheshimiwa Spika,*** APRM Tanzania iliandaa kitabu cha tathmini cha utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Awamu ya Sita katika masuala ya uchumi, kiitwacho *The Development Journey: Tanzania's Five-Year Milestones and Rolling Forward*. Kitabu hiki kinaangazia mafanikio makuu ya maendeleo ya uchumi yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita na kutoa mapendekezo ya kuendeleza mwenendo chanya katika hatua zijazo za maendeleo. Maandalizi ya kitabu hiki yalifanywa kwa ushirikiano wa karibu na taasisi za kitaaluma, hususan Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) na Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), ambapo taasisi hizi zilichangia kwa kutoa utaalamu wa utafiti, uchambuzi wa sera, na tathmini ya mwenendo wa maendeleo ya uchumi wa Taifa.

244. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, mwezi Februari 2026, ***APRM*** Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 35 wa Kawaida wa Jukwaa la Mpango wa Hiari wa Kujitathmini Afrika wa Wakuu wa Nchi na Serikali (*APRM Forum*) uliofanyika nchini Addis Ababa, Ethiopia. Katika Mkutano huo, Wakuu wa Nchi na Serikali walipokea na kujadili ripoti mbalimbali za tathmini ya Utawala Bora kutoka Nchi Wanachama wa APRM.

245. ***Mheshimiwa Spika***, miongoni mwa ripoti zilizowasilishwa ni Tathmini ya Pili ya Jamhuri ya Sierra Leone pamoja na Ripoti za Maeneo Maalum (*Targeted Reviews*) kutoka nchi za Togo, Ghana, Zimbabwe na São Tomé and Príncipe. Aidha, Jukwaa lilipokea taarifa za utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji *(NPoA)* kutoka Djibouti pamoja na *First Progress Report on the Targeted Review on Youth Unemployment* kutoka Namibia. Ripoti hizo zilibainisha maendeleo ya Nchi Wanachama katika kutekeleza mapendekezo ya APRM na kuimarisha Utawala Bora, usimamizi wa uchumi na maendeleo jumuishi Barani Afrika.

**Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim (SAS-CFR)**

246. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim kina jukumu la kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi katika masuala ya diplomasia; uhusiano wa kimataifa; stratejia; lugha za kigeni ambazo ni Kiarabu, Kifaransa, Kihispania, Kiingereza, Kichina, Kikorea na Kireno; usuluhishi wa migogoro; na ujenzi wa amani. Wanufaika wa mafunzo hayo ni pamoja na taasisi za Serikali, sekta binafsi, balozi na taasisi mbalimbali za kimataifa.

247. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kutoa mafunzo ya muda mfupi, kuendesha makongamano na mijadala ya wazi, Kituo hutoa pia mafunzo ya muda mrefu yanayohusu uhusiano wa kimataifa na diplomasia. Katika Mwaka wa Masomo 2025/2026 Kituo kimeweza kudahili jumla ya wanafunzi 1,797 wa kozi mbalimbali za muda mrefu ambapo kati ya hao 974 ni wanawake na 823 ni wanaume. Aidha, tarehe 6/1/2026 Kituo kilifanya mahafali ya 28 ambapo jumla ya wanafunzi 900 wa ngazi mbalimbali walihitimu masomo yao.

248. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo kiliendesha jumla ya kozi fupi 26 zilizotolewa kwa washiriki 1045. Nafurahi kukujulisha kuwa, miongoni mwa mafunzo hayo yalizihusisha pia Kamati za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Haya ni ya ni pamoja na yale yaliyotolewa kwa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama tarehe 11 Februari 2026, na Kamati ya Jumuiya za Kibunge ya tarehe 13 Februari, 2026. Aidha, Kituo pia huendesha mihadhara na makongamano inayohusu uhusiano wa kimataifa na diplomasia ili kutoa elimu kwa umma.

249. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2025/2026, Kituo kilipanga kukusanya na kutumia

**shilingi 8,278,516,000**. Kati ya fedha hizo **shilingi 3,428,450,000** ni mapato kutoka kwenye vyanzo vya ndani; na **shilingi 4,850,066,000** ni ruzuku kutoka Serikali Kuu. Ruzuku hiyo ilijumuisha **shilingi 1,500,000,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 3,350,066,000** kwa ajili ya mishahara.

250. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2026, Kituo kilikuwa kimekusanya **shilingi 5,871,555,863.01,** sawa **asilimia 71** ya mapato ya mwaka wa fedha 2025/2026. Kati ya fedha hizo, **shilingi 2,376,838,366.01** ni makusanyo kutoka vyanzo vya ndani sawa na **asilimia 69** ya lengo la mwaka; **shilingi 2,496,567,497.00** ni ruzuku ya mishahara kutoka Serikali Kuu sawa na **asilimia 75** ya lengo la mwaka; na **shilingi 998,150,000.00** ni ruzuku ya matumizi mengineyo kutoka Serikali Kuu, sawa na **asilimia 67** ya lengo la mwaka.

251. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2026, Kituo kimetumia **shilingi 5,060,222,093.29** sawa na **asilimia 86** ya fedha zilizokusanywa na kupokelewa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 1,667,448,618.70** ni kutoka vyanzo vya ndani, sawa na **asilimia 70** ya makusanyo ya vyanzo vya ndani; **shilingi 2,496,567,497** ni kwa ajili ya mishahara sawa na **asilimia 100** ya fedha za mishahara zilizopokelewa; na **shilingi 896,205,977.59** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, sawa na **asilimia 90** ya fedha za matumizi mengineyo zilizopokelewa.

**Kuimarisha Uchambuzi, Ufuatiliaji, Tathmini na Ukaguzi wa Ndani**

252. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua umuhimu wa kuimarisha ufuatiliaji na tathmini katika kufikia malengo na shabaha ilizojiwekea kwenye utekelezaji wa

majukumu. Hivyo, katika kipindi hiki, msisitizo uliendelea kuwekwa katika kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ndani na nje ya Wizara. Ufuatiliaji umefanyika katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024 pamoja na Mkakati wake wa utekelezaji na pia miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara.

253. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya tathmini ya mwisho ya Mpango Mkakati wake wa mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026 ili kubaini mafanikio yaliyopatikana pamoja na changamoto zilizopo na kuwezesha maandalizi ya Mpango Mkakati mpya unaoakisi mabadiliko ya kisera ikiwemo Dira 2050 na Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024. Mapendekezo ya tathmini hiyo yamejumuishwa katika Mpango Mkakati Mpya wa Wizara wa mwaka 2026/2027 - 2030/2031. Aidha, Wizara imeendelea kukiimarisha Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kwa kukiongezea rasilimali watu, bajeti na kujengea uwezo watumishi ikiwa ni hatua ya kuimarisha ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake.

254. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali za umma yanayozingatia thamani ya fedha na utendaji kazi wenye tija, Wizara kupitia Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani imefanya kaguzi kwenye maeneo ya usimamizi wa fedha, ununuzi, utawala na utekelezaji wa miradi ya maendeleo Makao Makuu, Balozi za Tanzania Nje na Konseli Kuu. Katika kipindi hiki jumla ya kaguzi 20 zilifanyika zikijumuisha kaguzi tano kwa Makao Makuu na kaguzi 15 kwa Balozi za Tanzania nje.

255. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia kaguzi hizo, ushauri na mapendekezo yalitolewa katika maeneo mbalimbali kama hatua ya kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi. Kitengo kimeweza pia kutoa ushauri juu ya masuala mbalimbali yaliyoelekezwa na Menejimenti ambayo yameboresha utendaji kazi wa Wizara.

256. ***Mheshimiwa Spika***, aidha, kufuatia kuanzishwa kwa Kitengo cha Mikakati na Siasa za Ulimwengu, Wizara imeendelea kufanya uchambuzi wa masuala ya kimkakati na siasa za ulimwengu pamoja na kutoa ushauri kwa Serikali na wadau wengine. Hatua hii inalenga kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa kwa kuzingatia mabadiliko na mivutano ya kisera na siasa za ulimwengu.

# 4.0 MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA UTATUZI WAKE

## 4.1 Mafanikio

257. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara na kwa kuzingatia Malengo ya Kimkakati ya Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024, mafanikio mbalimbali yamepatikana. Kwa muhtasari mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:

(i) Kuimarika kwa taswira na heshima ya Taifa letu katika nyanja za kimataifa;

(ii) Kuimarika kwa ushirikiano wa uwili ikiwemo kufanikisha upatikanaji wa rasilimali fedha, ujuzi na teknolojia kutoka nchi rafiki na fursa zitokanazo na Mikataba na Hati za Makubaliano zilizosainiwa;

(iii) Kuimarika kwa ushirikiano wa kikanda hususan kupitia utekelezaji wa Itifaki na Programu za Mtangamano zenye maslahi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa Taifa letu;

(iv) Kuimarika kwa ushirikiano wa kimataifa, ikiwemo kuwezesha ushiriki wa Tanzania katika ajenda zinazohitaji juhudi za pamoja kama vile masuala ya mazingira, mabadiliko ya tabianchi, nishati safi ya kupikia hususan kwa kinamama, kupambana na magonjwa ya mlipuko na uhalifu unaovuka mipaka;

(v) Kuwezesha Tanzania kupata nafasi za kimkakati katika jumuiya za kikanda na Kimataifa ikiwemo uteuzi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kushika nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika; Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nafasi ya Mwakilishi wa Ngazi ya Juu wa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika katika eneo la Pembe ya Afrika na Bahari ya Shamu na Mhe. *Balozi* Stephen Patrick Mbundi kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(vi) Kuimarika kwa mchango wa Watanzania Waishio Nje ya Nchi na Raia wa Nchi Nyingine Wenye Asili ya Tanzania katika maendeleo ya Taifa hususan katika sekta za fedha, uwekezaji, nyumba, kilimo na viwanda;

(vii) Kulinda usalama wa Watanzania walio nje ya nchi na kuwarejesha nyumbani salama kutoka kwenye maeneo yaliyokumbwa na vita na machafuko;

(viii) Kuimarika kwa utoaji wa elimu kwa umma hususan utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024 kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, machapisho na njia za kidijitali;

(ix) Kuimarika kwa mazingira ya utendaji kazi kwa kufanikisha uendelezaji wa milki ikiwemo ukarabati wa ofisi na makazi ya watumishi katika Balozi za Tanzania Nje; na

(x) Kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa kimkakati wa ujenzi wa kituo kipya na cha kisasa cha Mikutano cha Mlima Kilimanjaro (*Mt. Kilimanjaro International Convention Centre- MK-ICC*).

## 4.2 Changamoto na Hatua za Utatuzi Wake

258. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio yaliyoainishwa hapo juu, bado Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake kama ifuatavyo:

(i) Baadhi ya Nchi Wanachama katika Jumuiya za Kikanda kutoheshimu baadhi ya Mikataba na Makubaliano ikiwemo kutolipa michango yao ya kibajeti kwa wakati. Hatua hii inaathiri uratibu na ushiriki wetu katika utekelezaji wa Programu za Mtangamano wa Kikanda;

(ii) Baadhi ya wadau ikiwemo sekta binafsi kutochangamkia ipasavyo fursa zitokanazo na utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kupitia ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa; (mathalan baadhi ya wafanyabiashara kutokuwa na uwezo wa kusambaza bidhaa kwa wakati na kwa kiwango kinachotakiwa wakati wote, baadhi ya bidhaa kutokuwa na ubora unaotakiwa na zinazokidhi viwango vya masoko ya kimataifa;

(iii) Kuzorota kwa hali ya amani na usalama katika baadhi ya nchi ndani na nje ya ukanda wa Afrika na hivyo kuathiri utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024;

(iv) Mabadiliko ya mwelekeo wa hali ya kisera na mvutano katika siasa za kidunia. Hali hii imepelekea kutotabirika kwa mwelekeo wa sera katika uhusiano wa kimataifa; na

(v) Kasi ndogo ya kuridhia na kutekeleza Makubaliano ya uwili, kikanda na kimataifa. Hivyo kusababisha kuchelewa kufanikisha malengo ya makubaliano.

259. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto hizo Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa kushirikiana na wadau wengine ndani na nje ya Serikali kama ifuatavyo:

(i) Katika kukabiliana na changamoto ya baadhi ya Nchi Wanachama kutoheshimu makubaliano na mikataba ya kikanda, Wizara imeendelea kutumia njia mbalimbali za kidiplomasia na inapolazimu kuhimiza matumizi ya vikwazo vilivyowekwa katika ngazi ya Jumuiya ili kushinikiza nchi hizo kulipa michango yake kwa wakati. Aidha, Tanzania imewezesha mabadiliko ya kanuni za uchangiaji katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuwezesha nchi husika kuwajibika na kulipa michango yake kwa wakati;

(ii) Katika kukabiliana na changamoto ya baadhi ya wadau kutokuchangamkia ipasavyo fursa za ushirikiano, Wizara imeendelea kutumia mbinu mbadala ikiwemo kuongeza matumizi ya teknolojia kama vile mitandao ya kijamii na machapisho ya kidijitali katika kutoa elimu kwa umma. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza diplomasia ya umma (*public diplomacy*) ili kuendana na mazingira ya sasa na ya baadaye;

(iii) Kuhusu changamoto ya amani na usalama, Wizara imeendelea kuratibu juhudi za Tanzania katika kusuluhisha migogoro kupitia ushirikiano wa uwili, juhudi za kikanda hususan katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Nchi Zilizopo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA). Aidha, Wizara imeendelea kuratibu na kushiriki kikamilifu katika kuunga mkono juhudi za Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa kuleta suluhu ya migogoro kwa njia za kidiplomasia;

(iv) Kuhusu mabadiliko ya mwelekeo wa hali ya kisera na mvutano katika siasa za kidunia, Tanzania imeendelea kuzingatia misingi ya Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024 ikiwemo msingi wa kutofungamana na upande wowote katika ushirikiano wa kimataifa;

(v) Kuhusu kasi ndogo ya kuridhia na kutekeleza Makubaliano ya uwili, kikanda na kimataifa; Tanzania imeendelea kutumia majukwaa na mbinu za kidiplomasia kuharakisha utekelezaji wake. Aidha, Wizara imeanzisha mfumo wa kidigitali wa uratibu na usimamizi wa mikataba na makubaliano ya kimataifa.

## 5.0 SHUKRANI

260. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuonesha dhamira thabiti na jitihada za kipekee katika kuimarisha uhusiano wa kimataifa, diplomasia pamoja na kuendelea kushirikiana kwa karibu na wadau wa maendeleo.

261. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa washirika wa maendeleo, wadau wote wa maendeleo, pamoja na jumuiya za kikanda na kimataifa kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya uwili, kikanda na kimataifa na kuchangia maendeleo endelevu kwa Taifa letu. Ninaamini kwa pamoja tunaweza kufikia mafanikio makubwa zaidi kwa manufaa ya Watanzania wote.

262. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee, naomba kutumia fursa hii kuzishukuru nchi zifuatazo: Afrika Kusini, Algeria, Angola, Australia, Austria, Azerbaijan, Barbados, Brazil, Brunei, Botswana, Burundi, Canada, China, Comoros, Cuba, Cyprus, Croatia, Denmark, Ethiopia, Eswatini, Finland, Georgia, Hispania, Hungary, Indonesia, India, Israel, Italia, Iran, Ireland, Jamhuri ya Czech, Jamhuri ya Korea, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea, Jamaika, Japan, Kenya, Kosovo, Kuwait, Latvia, Lesotho, Madagascar, Malawi, Malaysia, Malta, Marekani, Mauritius, Mexico, Misri, Morocco, Msumbiji, Namibia, New Zealand, Nigeria, Norway, Oman, Pakistan, Poland, Qatar, Romania, Rwanda, Serbia, Singapore, Sri Lanka, Thailand, Tunisia, Ubelgiji, Saudi Arabia, Saharawi, Samoa, Shelisheli, Slovenia, Sudan, Sudani Kusini, Sweden, Ufaransa, Ufilipino, Uganda, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Ukraine, Umoja wa Falme za

Kiarabu, Ureno , Urusi, Uswisi, Uturuki, Viet Nam, Zambia na Zimbabwe.

263. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, naomba kutoa shukrani kwa African Capacity Building Foundation (ACBF); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Benki ya Dunia (WB); *Investment Climate Facility for Africa*; Benki ya Exim ya China; Benki ya Exim ya India; Benki ya Exim ya Korea; Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD); Mfuko wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Uchumi wa Korea (EDCF); Mfuko wa Maendeleo wa China na Afrika (CAD Fund); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DfID); Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi (ADFD); Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (Kuwait Fund); Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA) na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA).

264. ***Mheshimiwa Spika,*** pia natoa shukrani kwa Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD); Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD); Shirika la Kimataifa la Kuzuia Matumizi ya Silaha za Kemikali (OPCW); Shirika la Maendeleo Ubelgiji (ENABEL); Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Italia (AICS); Shirika la Maendeleo la Uturuki (TIKA); Jumuiya ya Nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki (OACPS); Ofisi ya Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN RCO); Mfuko wa Kukuza Mtaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF); Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA); na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na UKIMWI (UNAIDS); Mfuko wa Maendeleo wa *Saudi Fund* (SFD).

265. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, natoa shukrani kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR); Shirika la Kazi

Duniani (ILO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamaji (IOM); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF); Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Israel (MASHAV); Shirika la Misaada la Indonesia (IndoAid); Shirika la Ushirikiano wa Kiutaalam na Kiuchumi la India (ITEC); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA); Shirika la Misaada la Marekani (USAID); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea (KOICA); Shirika la Kimataifa la Ushirikiano wa Maendeleo la China (CIDCA); Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO); na Taasisi ya Kimataifa ya Afya ya Korea (KOFIH).

266. ***Mheshimiwa Spika,*** mashirika mengine ni Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wanawake (UNWOMEN); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD); Shirika la Umoja wa Mataifa Kuhusu Madawa ya Kulevya na Uhalifu (UNODC); Umoja wa Ulaya (EU); Shirika la Afya Duniani (WHO); na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP). Vilevile, napenda kuwashukuru Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika (BADEA) na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB).

267. ***Mheshimiwa Spika,*** mashirika mengine ni Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GiZ); Global Fund; International Committee of the Red Cross; International Federation of the Red Cross and Red Crescent Societies; Khalifa Fund for Enterprise Development (Khalifa Fund); Medecins Sans Frontieres (MSF); Mfuko wa Dunia wa Wanyama Pori (WWF); Taasisi ya Elimu ya Uturuki *(Turkish Maarif Foundation)*; Aga Khan Foundation (AKDN) The Association of European Parliamentarians with Africa; The Bill and Melinda Gates Foundation; TradeMark Africa; Umoja wa Posta Duniani (UPU); International Telecommunication Union (ITU)

Umoja wa Posta Afrika (PAPU); Taasisi ya Ushirikiano wa Kitaaluma ya Malaysia (MTCP); Taasisi ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Thailand (Thailand International Cooperation Agency); Baraza la India la Mahusiano ya Utamaduni (ICCR) pamoja na mifuko na mashirika mengine ya misaada.

## 6.0 MAPENDEKEZO YA VIPAUMBELE NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### 6.1 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

268. ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 vitaendelea kutekelezwa kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa: Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2026/2027 - 2030/31).

269. ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele pia vitazingatia Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (2021 – 2026); Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika wa mwaka 1992; Ajenda ya Mwaka 2030 ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu; Ajenda ya Mwaka 2063 ya Umoja wa Afrika; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya Mwaka 2050; Dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2050; na mikataba mingine ya Jumuiya za Kikanda na Kimataifa.

270. ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya Wizara vitaongozwa na maelekezo ya viongozi wakuu wa kitaifa pamoja na ushauri unaotolewa na Bunge. Kwa muktadha huo, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 vitakuwa kama ifuatavyo:

(i) Kuendelea kuimarisha uratibu na ushirikiano wa uwili, Kikanda na Kimataifa;

(ii) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024 hususan utekelezaji wa diplomasia ya uchumi;

(iii) Kulinda Taswira, heshima na kutetea maslahi ya Taifa letu katika nyanja ya kimataifa; na

(iv) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi wa Wizara, kuimarisha utawala bora na rasilimali watu pamoja na kutekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara na taasisi zake.

## 6.2 Vipaumbele vya Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

### Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC)

271. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 kituo kinatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kuendelea kuvutia na kutoa huduma za mikutano zinazokidhi viwango vya kimataifa ili kukuza jina la Tanzania katika sekta ya Utalii wa Mikutano duniani na kuvutia wawekezaji katika sekta hiyo;

(ii) Kuendelea kuitangaza Tanzania kupitia diplomasia ya kiuchumi, kuboresha mbinu za masoko, kuongeza idadi ya mikutano na shughuli zinazoingizia kituo mapato; na

(iii) Kuendelea kushirikiana na sekta binafsi na mashirika ya kimataifa katika kufikia malengo yake.

**Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim (SAS-CFR)**

272. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 kituo kinatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kuendelea kutoa mafunzo ya uhusiano wa kimataifa na diplomasia na lugha ya Kiswahili kwa wageni;

(ii) Kuendelea kutafiti maeneo ya uhusiano wa kimataifa na diplomasia;

(iii) Kuendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia;

(iv) Kuendelea kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi wa kituo;

(v) Kuendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa wadau mbalimbali ikiwemo Serikali na taasisi zake; na

(vi) Kuendelea kukitangaza kituo kitaifa na kimataifa.

**Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Utawala Bora (APRM)**

273. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 APRM Tanzania inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

(i) Kuendelea kufanya tafiti katika maeneo ya usimamizi wa uchumi, uendeshaji wa mashirika ya biashara, utoaji wa huduma za kijamii, demokrasia na siasa na utayari wa nchi katika kukabiliana na majanga;

(ii) Kuhuisha mbinu za tafiti ikiwa ni pamoja na kuboresha viashiria vya tafiti, kuimarisha matumizi ya teknolojia katika utekelezaji wa mpango na kupanua wigo wa kufanya tafiti; na

(iii) Kuendelea kujenga uwezo wa watumishi na wadau muhimu katika kufanya utekelezaji wa mpango wa APRM.

## 7.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### Maduhuli ya Serikali

274. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya Serikali ya kiasi cha **shilingi 1,511,000,000** kutoka vyanzo mbalimbali vilivyopo ofisi za makao makuu na Balozi za Tanzania Nje ya Nchi. Vyanzo hivyo vya mapato vinajumuisha upangishaji wa nyumba za Serikali zilizopo nje ya nchi, ukodishaji wa kumbi za mikutano na zoezi la kuthibitisha nyaraka. **Jedwali Na. 2** linaainisha mchanganuo wa makadirio ya mapato ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Jedwali Na. 2: Makadirio ya Maduhuli ya Wizara kwa Mwaka 2026/2027**

| KIFUNGU NA. | JINA LA KIFUNGU | VYANZO | KIASI (TZS) |
|---|---|---|---|
| **A. MAKAO MAKUU** | | | |
| 1001 | Administration and Human Resource Management | Miscellaneous receipts | 180,000,000 |
| 1003 | Foreign Affairs Zanzibar | Miscellaneous receipts | 114,547,000 |
| **JUMLA NDOGO – MAKAO MAKUU** | | | **294,547,000** |
| **B. BALOZI ZA TANZANIA NJE YA NCHI** | | | |
| 2001 | Addis Ababa | Miscellaneous receipts | 6,119,251 |
| 2002 | Berlin | Miscellaneous receipts | 5,250,000 |
| 2003 | Cairo | Miscellaneous receipts | 10,500,000 |
| 2004 | Kinshasa | Miscellaneous receipts | 1,525,000 |
| 2005 | Abuja | Miscellaneous receipts | 525,000 |
| 2006 | London | Miscellaneous receipts | 11,300,000 |

| KIFUNGU NA. | JINA LA KIFUNGU | VYANZO | KIASI (TZS) |
|---|---|---|---|
| 2007 | Lusaka | Rent | 54,554,432 |
| | | Miscellaneous receipts | 525,000 |
| 2008 | Maputo | Rent | 26,636,075 |
| | | Miscellaneous receipts | 3,457,602 |
| 2009 | Moscow | Miscellaneous receipts | 5,675,000 |
| 2010 | New Delhi | Miscellaneous receipts | 525,000 |
| 2011 | UN - New York | Miscellaneous receipts | 12,000,000 |
| 2012 | Ottawa | Miscellaneous receipts | 1,050,000 |
| 2013 | Paris | Rent | 343,096,498 |
| | | Miscellaneous receipts | 1,266,000 |
| 2014 | Beijing | Miscellaneous receipts | 525,000 |
| 2015 | Rome | Miscellaneous receipts | 6,852,636 |
| 2016 | Stockholm | Miscellaneous receipts | 3,990,000 |
| 2017 | Tokyo | Miscellaneous receipts | 1,050,000 |
| 2018 | Washington D.C | Miscellaneous receipts | 5,250,000 |
| 2019 | Brussels | Miscellaneous receipts | 6,150,000 |
| 2020 | UN - Geneva | Miscellaneous receipts | 5,150,000 |
| 2021 | Kampala | Miscellaneous receipts | 630,000 |
| 2022 | Harare | Rent | 88,644,780 |
| | | Miscellaneous receipts | 840,000 |
| 2023 | Nairobi | Miscellaneous receipts | 525,000 |
| 2024 | Riyadh | Miscellaneous receipts | 5,775,000 |
| 2025 | Pretoria | Miscellaneous receipts | 525,000 |
| 2026 | Kigali | Miscellaneous receipts | 1,575,000 |
| 2027 | Abu Dhabi | Miscellaneous receipts | 121,861,285 |

| KIFUNGU NA. | JINA LA KIFUNGU | VYANZO | KIASI (TZS) |
|---|---|---|---|
| 2028 | Bujumbura | Miscellaneous receipts | 525,000 |
| 2029 | Muscat | Miscellaneous receipts | 440,000,000 |
| 2030 | Lilongwe | Miscellaneous receipts | 525,000 |
| 2031 | Brasilia | Miscellaneous receipts | 525,000 |
| 2032 | Kuala Lumpur | Miscellaneous receipts | 525,000 |
| 2033 | The Hague | Miscellaneous receipts | 4,200,000 |
| 2034 | Moroni | Miscellaneous receipts | 525,000 |
| 2035 | Kuwait City | Miscellaneous receipts | 2,100,000 |
| 2036 | Algiers | Miscellaneous receipts | 1,575,000 |
| 2037 | Ankara | Miscellaneous receipts | 15,750,000 |
| 2038 | Khartoum | Miscellaneous receipts | 500,000 |
| 2039 | Seoul | Miscellaneous receipts | 9,250,000 |
| 2040 | Tel Aviv | Miscellaneous receipts | 1,050,000 |
| 2041 | Doha | Miscellaneous receipts | 4,200,000 |
| 2042 | Havana | Miscellaneous receipts | 525,000 |
| 2043 | Windhoek | Miscellaneous receipts | 525,000 |
| 2044 | Jakarta | Miscellaneous receipts | 400,000 |
| 2045 | UN – Vienna | Miscellaneous receipts | 404,441 |
| **JUMLA NDOGO – BALOZI ZA TANZANIA** | | | **1,216,453,000** |
| **JUMLA KUU** | | | **1,511,000,000** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki*

**Matumizi ya Kawaida**

275. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara imepanga kutumia kiasi cha **shilingi 312,961,378,000.** Kati ya fedha hizo **shilingi 290,299,192,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 22,662,186,000** kwa ajili ya mishahara ya watumishi waliopo Makao Makuu ya Wizara na Balozi za Tanzania.

276. ***Mheshimiwa Spika,*** bajeti ya matumizi mengineyo inajumuisha **shilingi 1,257,428,928** kwa ajili ya Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini Katika Masuala ya Utawala Bora na Demokrasia; **shilingi 1,400,000,000** kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu; **shilingi 1,500,000,000** kwa ajili ya Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim; na **shilingi 280,000,000** kwa ajili ya Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika.

277. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, bajeti ya mishahara inajumuisha shilingi **3,347,228,000** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim na **shilingi 567,871,929** kwa ajili ya mishahara ya APRM.

**Matumizi ya Maendeleo**

278. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara imepanga kutumia fedha kiasi cha **shilingi 46,365,026,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Fedha hizo zinajumuisha **shilingi 15,000,000,000.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa makao makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu jijini Arusha; **shilingi 200,000,000.00** kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Ofisi za Wizara Dar es Salaam; **shilingi 5,000,000,000.00** kwa

ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Afrika ya Usuluhishi wa Masuala ya Rushwa; **shilingi 1,500,000,000.00** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la vyumba tisa (9) vya mihadhara katika Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim jijini Dar es Salaam; **shilingi 10,000,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi za Wizara katika eneo la Kisakasaka Zanzibar; **shilingi 13,840,026,000.00** kwa ajili ya kugharamia ujenzi, ukarabati na ununuzi wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi balozini. Vilevile, Wizara imetengewa kiasi cha **shilingi 825,000,000.00** kutoka wadau wa maendeleo kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa diplomasia ya Uchumi.

## 8.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha(AICC)**

279. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/2027 AICC imepanga kukusanya mapato kiasi cha **shilingi 32,664,408,042** kutokana na vyanzo vya ndani. Mapato hayo yatatumika kugharamia uendeshaji wa Kituo ikiwemo kuhudumia mikutano, kulipa mishahara ya watumishi na kutekeleza miradi ya maendeleo ya ukarabati wa kumbi za mikutano, majengo ya ofisi na makazi, upanuzi wa huduma na ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali ya AICC pamoja na ununuzi na usimikaji wa vifaa vya TEHAMA na samani katika vyumba vya mikutano.

**Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim(SAS-CFR)**

280. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/2027 Kituo kinakadiria kupokea na kutumia fedha kiasi cha **shilingi 8,565,403,396**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 3,283,900,000** zitatokana na mapato kutoka vyanzo vya ndani; na **shilingi 5,281,503,396** ni ruzuku kutoka Serikali Kuu itakayojumuisha **shilingi 1,500,000,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **shilingi 3,781,503,396** kwa ajili ya mishahara kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 3**.

**Jedwali Na. 3: Makisio ya Mapato na Matumizi ya SAS-CFR kwa mwaka 2026/2027**

| NA. | MAELEZO | BAJETI (SH.) |
|---|---|---|
| (i) | Ruzuku ya Mishahara | 3,781,503,396 |
| (ii) | Ruzuku ya Matumizi Mengineyo | 1,500,000,000 |
| (iii) | Mapato ya Ndani | 3,283,900,000 |
| **JUMLA KUU** | | **8,565,403,396** |

***Chanzo:*** *Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim*

**Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Utawala Bora(APRM)**

281. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 APRM Tanzania inakadiria kupokea na kutumia fedha kiasi cha **shilingi 1,782,143,928.** Kati ya fedha hizo, **shilingi 567,871,929** ni ruzuku ya mishahara kutoka Serikali Kuu; na **shilingi 1,214,271,999** ni ruzuku ya matumizi mengineyo kutoka Serikali Kuu.

## 9.0 HITIMISHO

282. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 359,326,404,000**. Kati ya fedha hizo **shilingi 312,961,378,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 46,365,026,000** ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

283. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kuhitimisha kwa kukushukuru tena wewe binafsi, kwa jinsi unavyoendesha vikao vya Bunge kwa weledi na umahiri wa hali ya juu. Aidha, kwa niaba ya Wizara napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao waliyoitoa kwa Wizara yangu.

284. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho Na. 1: Orodha ya Mikataba na Hati za Makubaliano kati ya Tanzania na Nchi Nyingine katika Mwaka wa Fedha 2025/2026

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| 1. | Hati ya Makubaliano kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Cyprus kuhusu Mashauriano ya Kisiasa<br><br>*Memorandum of Understanding between the Ministry of Foreign Affairs and East African Cooperation of the United Republic of Tanzania and the Ministry of Foreign Affairs of the Republic of Cyprus on Cooperation and Bilateral Political Consultations* | 09 Julai, 2025 |
| 2. | Hati ya Makubaliano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Cyprus kuhusu Utambuzi wa Vyeti vya Mabaharia<br><br>*Memorandum of Understanding between the United Republic of Tanzania and the Republic of Cyprus on recognition of certificates issued under the provisions of the International Convention on standards of training, certification and Watch keeping for seafarers 1978 as amended* | 09 Julai, 2025 |
| 3. | Hati ya Makubaliano kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Kampuni ya Utafiti na Maendeleo ya Petroli ya Nigeria kuhusu Kuendeleza Kitalu cha Kaskazini cha Rasi ya Mnazi | 18 Julai, 2025 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
| --- | --- | --- |
| | *Memorandum of Understanding between the Tanzania Petroleum Development Corporation and First Exploration and Petroleum Development Company Limited of Nigeria to establish a structured Framework for the Collaboration in Evaluating and Progressing the exploration license for the Mnazi Bay North Block* | |
| 4. | Hati ya Makubaliano kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Elimu ya Jamhuri ya Belarus kuhusu Masuala ya Elimu<br><br>*Memorandum of Understanding between The Ministry of Education, Science and Technology of the United Republic of Tanzania and The Ministry of Education of the Republic of Belarus on Cooperation in the Field of Education* | 22 Julai, 2025 |
| 5. | Hati ya Makubaliano kati ya Wizara ya Kilimo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Kilimo na Chakula ya Jamhuri ya Belarus kuhusu Masuala ya Kilimo<br><br>*Memorandum of Understanding between the Ministry of Agriculture of the United Republic of Tanzania and the Ministry of Agriculture and Food of the Republic of Belarus on Cooperation in Agricultural Field* | 22 Julai, 2025 |
| 6. | Hati ya Makubaliano kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Belarus kuhusu Mashauriano ya Kisiasa<br><br>*Memorandum of Understanding between The Ministry of Foreign Affairs and East* | 22 Julai, 2025 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| | *African Cooperation of the United Republic of Tanzania and the Ministry of Foreign Affairs of the Republic of Belarus on Political Consultations* | |
| 7. | Mkataba wa Ushirikiano kati ya Chemba ya Biashara na Viwanda ya Jamhuri ya Belarus na Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania<br><br>*Agreement of cooperation between the Belarusian Chamber of Commerce and Industry (Republic of Belarus) and the Tanzania Chamber of Commerce Industry and Agriculture (United Republic of Tanzania)* | 22 Julai, 2025 |
| 8. | Azimio la Pamoja la kuanzisha Kamati ya Pamoja ya Biashara kati ya Wizara ya Biashara ya Jamhuri ya Uturuki na Wizara ya Viwanda na Biashara ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania<br><br>*The Joint Declaration on the Establishment of the Joint Trade Committee (JTC) between the Ministry of Trade of the Republic of Turkiye and the Ministry of Industry and Trade of the United Republic of Tanzania* | 23 Julai, 2025 |
| 9. | Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Rwanda kuhusu Masuala ya Kilimo<br><br>*Memorandum of Understanding between the Government of the Republic of Rwanda and the Government of the United Republic of Tanzania on cooperation in the field of Agriculture* | 26 Julai, 2025 |
| 10. | Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Rwanda kuhusu | 26 Julai, 2025 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| | Kuanzisha Ofisi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Kigali, Rwanda<br><br>*Memorandum of Understanding between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Rwanda for the establishment and operationalization of Tanzania Ports Authority's liaison office in Kigali, Rwanda.* | |
| 11. | Hati ya Makubaliano kati ya Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania na Kituo cha Kimataifa cha Ubia cha Nguvu za Atomu cha India<br><br>*Memorandum of Understanding between Tanzania Atomic Energy Commission (TAEC) and the Global Centre for Nuclear Energy Partnership GCNEP of India* | 11 Agosti, 2025 |
| 12. | Hati ya Makubaliabo kati ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Jamhuri ya Angola na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Usalama wa Raia na Zimamoto<br><br>*Memorandum of Understanding between the Ministry of Interior of the Republic of Angola and the Ministry of Home Affairs of the United Republic of Tanzania in the Field of Civil Protection and Firefighting* | 13 Agosti, 2025 |
| 13. | Mkataba kati ya Baraza la Maendeleo ya Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya 4 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Makao Makuu ya Sekretariati ya Baraza la Maendeleo ya Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya 4 kuwa Nchini Tanzania.<br><br>*Agreement between the African Union Sports Council Development Region 4 and the Government of the United Republic of* | 20 Agosti, 2025 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| | *Tanzania for the Hosting of the African Union Sports Council Development Region 4 Secretariat* | |
| 14. | Hati ya Makubaliano kati ya Wizara ya Katiba na Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Sheria ya Japan<br><br>*Memorandum of Understanding between the Ministry of Constitutional and Legal Affairs of the United Republic of Tanzania and the Ministry of Justice of Japan* | 21 Agosti, 2025 |
| 15. | Hati ya Ushirikiano kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Ardhi, Miundombinu, Usafirishaji na Utalii ya Japan katika Masuala ya Kuendeleza Rasilimali Watu katika Sekta ya Ujenzi<br><br>*Memorandum of Cooperation (MOC) between the Prime Ministers Office Labour, Youth, Employment and Persons with Disability of Tanzania and the Ministry of Land, Infrastructure, Transport and Tourism of Japan on Cooperation in Human Resources Development in Construction Sector* | 21 Agosti, 2025 |
| 16. | Hati ya Makubaliano baina ya Wizara ya Usafirishaji ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya Toyota Tshisho ya Japan katika Sekta ya Usafirishaji<br><br>*Memorandum of Understanding between the Ministry of Transport of the United Republic of Tanzania and Toyota Tshisho Cooperation in Cooperation on Transport field* | 22 Agosti, 2025 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
| --- | --- | --- |
| 17. | Hati ya Makubaliano kati ya Jeshi la Magereza Tanzania na MGM Muthu Agriculture (MGM) ya India kuhusu Ushirikiano katika Maendeleo ya Kilimo na Ufugaji katika Mashamba ya Magereza nchini<br><br>*Memorandum of Understanding between Tanzania Prison Service (TPS) and MGM Muthu Agriculture (MGM) of India for Cooperation on Farming and Livestock Development in Tanzania Prison Farms* | 12 Septemba, 2025 |
| 18. | Mkataba wa Uwenyeji kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation kuhusu Uboreshaji, Uendeshaji, Ukarabati, Utawala na Ugharamiaji wa Reli ya TAZARA<br><br>*Host Government Agreement between the Government of the United Republic of Tanzania and China Civil Engineering Construction Corporation Linkfuture Investment Ltd Tazara Revitalization Tanzania Limited relating to Public Private Partnership for the Rehabilitation, Renovation, Operation, Maintenance, Management and Financing of the Tanzania- Zambia Railway Project* | 29 Septemba, 2025 |
| 19. | Hati ya Makubaliano ya kuanzisha Tume ya Pamoja ya Ushirikiano kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Uturuki<br><br>*Memorandum of Understanding on the Establishment of the Joint Commission for Bilateral Cooperation between the Ministry of Foreign Affairs and East African* | 16 Septemba, 2025 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| | *Cooperation of the United Republic of Tanzania and the Ministry of Foreign Affairs of the Republic of Turkiye* | |
| 20. | Hati ya Makubaliano baina ya Shirika la Maendeleo ya Petroli la Tanzania na PJSC Gazprom kuhusiana na ushirikiano katika masuala mengine ya gesi asilia.<br><br>*Memorandum of Understanding between Tanzania Petroleum Development Cooperation and PJSC Gazprom on Cooperation in other natural gas-related areas.* | 07 October, 2025 |
| 21. | Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Uchukuzi na Chemba ya Maendeleo ya Biashara ya Jamhuri ya Czech kuhusu Kuanzisha Mpango Mkakati wa Kuboresha Miundombinu ya Usafirishaji Nchini Tanzania<br><br>*Memorandum of Understanding between the Government of the United Republic of Tanzania through the Ministry of Transport and Czech Development Chamber of Commerce for establishing a durable strategic framework for modernizing Transportation Infrastructure in the United Republic of Tanzania.* | 07 Novemba, 2025 |
| 22. | Mkataba wa Ushirikiano kati ya Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Chuo Kikuu cha Misitu cha Saint Petersburg kuhusu Mafunzo na Kubadilishana Ujuzi na Uzoefu katika Utawala<br><br>*Cooperation Agreement between the Sokoine University of Agriculture and Federal State Budgetary Educational Institution of Higher Education Saint Petersburg State Forest Technical University* | 19 Novemba, 2025 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| | *on Training, Academic Administrative Exchange.* | |
| 23. | Hati ya Makubaliano ya Utambuzi wa Pamoja wa Vyeti vya Mabaharia kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Taifa la Qatar<br><br>*Memorandum of Understanding on Mutual Recognition of Seafarers Certificates between the United Republic of Tanzania and the State of Qatar* | 24 Novemba, 2025 |
| 24. | Hati ya Ushirikiano ya Makubaliano kati ya Wakala wa Dawa na Vifaa Tiba (National Agency for Pharmaceuticals Products (ANPP) ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<br>*Memorandum of Understanding between National Agency for Pharmaceuticals Products (ANPP) of the Peoples Democratic Republic of Algeria and Tanzania Medicines and Medical Devices Authority (TMDA) of the United Republoic of Tanzania.* | 28 Novemba, 2025 |
| 25. | Mkataba wa Utambuzi wa Pamoja wa Matokeo ya Vipimo kati ya Wakala wa Vipimo Tanzania na Wakala wa Vipimo Zambia<br><br>*Mutual Recognition Framework Agreement for the Harmonisation of Legal Metrology and Measurement Standards between The Zambia Metrology Agency (ZMA) and The Weights and Measures Agency of Tanzania (WMA)* | 11 Desemba, 2025 |
| 26. | Hati ya Makubaliano kati ya Kituo cha Utangamano wa Kikanda na Maendeleo cha Mananga cha Eswatini na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini cha | 13 Desemba, 2025 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| | Tanzania kuhusu Kubadilishana Maarifa, Ujuzi, Utafiti na Mafunzo ya Muda Mfupi<br><br>*Memorandum of Understanding between Mananga Centre for Regional Integration and Management Development of Eswatini and Institute of Rural Development Planning of Tanzania on sharing knowledge and resources in innovation, research, consultancy, short courses, development planning and dissemination of knowledge and information that are better suited to user requirements* | |
| 27. | Hati ya Makubaliano kati ya Chuo Kikuu cha Eswatini na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini cha Tanzania kuhusu Kubadilishana Maarifa, Mafunzo, Utafiti na Ushauri<br><br>*Memorandum of Understanding between University of Eswatini and Institute of Rural Development Planning on sharing knowledge and resources in innovation, research, consultancy, short courses, development planning and dissemination of knowledge and information that are better suited to user requirements* | 13 Desemba, 2025 |
| 28. | Hati ya Makubaliano kati ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania na Chuo Kikuu cha Misitu cha Saint Petersburg kuhusu Mafunzo, Utafiti na Matumizi ya Teknolojia ya Kisasa katika Kuimarisha Uhifadhi wa Misitu nchini Tanzania<br><br>*Memorandum of Understanding between Tanzania Forest Services Agency and Saint Petersburg State Forest Technical University on collaboration on Training, Research and use of Advanced Technologies to support* | 18 Desemba, 2025 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| | *Forest Conservation and Management in Tanzania* | |
| 29. | Hati ya Makubaliano baina ya Serikali ya India na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Masuala ya Tiba Asili<br><br>*Memorandum of Understanding between the Government of India and the Government of the United Republic of Tanzania on Cooperation in the Field of Traditional Medicine and Indian AYUVERDA* | 19 Desemba, 2025 |
| 30. | Mkataba wa Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi kuhusu Urahisishaji wa Kufanya Biashara kati ya Malawi na Tanzania<br><br>*Agreement between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Malawi for Simplified Trade Regime* | 16 Februari, 2026 |
| 31. | Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Somalia kuhusu Usimamizi wa Masuala ya Uhamiaji.<br><br>*Memorandum of Understanding between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Federal Republic of Somalia on Cooperation in Immigration Management* | 16 Februari, 2026 |
| 32. | Hati ya Makubaliano baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda ya Uendelezaji wa Reli ya SGR | 13 Machi, 2026 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| | kutoka ISAKA-LUSAHUNGA-MURONGO/KIKAGATI-MPONDWE<br><br>*Memorandum of Understanding between the United Republic of Tanzania and the Republic of Uganda for the Development of ISAKA-LUSAHUNGA-MURONGO/KIKAGATI-MPONDWE Standard Gauge Railway* | |
| 33. | Hati ya Makubaliano kati ya Chuo Kikuu cha Limerick cha Ireland na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusiana na udhamini wa masomo wa Samia kwa wanafunzi wa Sayansi ya Data iliyoendelea, Akili Mnemba (AI) na Sayansi Shirikishi (SSE DS/AI+) kwa wanafunzi wanaosoma programu za Shahada katika Chuo kikuu cha Limerick.<br><br>*Memorandum of Agreement between the University of Limerick and the Ministry of Education, Science and Technology (moest) of the United Republic of Tanzania regarding Samia Scholarship extended Data Science, AI and allied Sciences (sse ds/ai+) Students undertaking Degree Programmes at the University of Limerick.* | 26 March 2026 |
| 34. | Hati ya Makubaliano kati ya Wizara ya Uchukuzi ya Shirikisho la Urusi na Wizara ya Uchukuzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu usafirishaji na upitishaji wa mizigo.<br><br>*Memorandum of Understanding between the Ministry of Transport of the Russian Federation and the Ministry of Transport of* | 03 Aprili, 2026 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| | *the United Republic of Tanzania in the Field of Transport and Transit.* | |
| 35. | Mkataba kati ya *Miss World Limited* na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mwenyeji wa Mashindano ya 74 ya Urembo duniani.<br>*74th Miss World Festival Staging Agreement between Miss World Limited and the Ministry of Information, Culture, Arts and Sports of the United Republic of Tanzania.* | 20 Aprili, 2026 |
| 36. | Mkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Belarus na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzisha Tume ya Ushirikiano ya pamoja ya Biashara na Uchumi<br>*Agreement between the Government of the Republic of Belarus and the Government of the United Republic of Tanzania on establishement of a joint Committee on Trade and Economic Cooperation* | 29 April, 2026 |
| 37. | Hati ya Makubaliano kuhusu ushirikiano katika Sekta ya Reli kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yay a Jamhuri ya Kenya.<br>*Memorandum of Understanding between the Government of the Republic of Kenya and the Government of the United Republic of Tanzania for the Development, Operation and Management of Railway Networks* | 04 Mei, 2026 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| 38. | Mkataba kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kenya kwa Ajili ya Kufanya Upembuzi Yakinifu kwa Ajili ya Ujenzi wa Mradi wa Bomba la Gesi kutoka Dar es Salaam hadi Mombasa Kenya<br><br>*Bilateral Agreement between the Government of the United Republic of Tanzania Republic and the Government of the Republic of Kenya and the Government relating to conducting a feasibility Study for the development of Natural Gas Export Project from Dar es Salaam, Tanzania to Mombasa, Kenya.* | 04 Mei, 2026 |
| 39. | Mkataba kuhusu Kusaidiana katika masuala ya Jinai baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya.<br><br>*Agreement on Mutual Legal Assistance in criminal matters between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Kenya.* | 04 Mei, 2026 |
| 40. | Hati ya Makubaliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya katika masuala ya Kilimo.<br><br>*Memorandum of Understanding between the Government of the United Republic of Tanzania represented by the Ministry of Agriculture and Government of the Republic of Kenya represented by the Ministry of* | 04 Mei, 2026 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| | *Agriculture and Livestock Development on Cooperation in the field of Agriculture* | |
| 41. | Rasimu ya Mkataba kuhusu Utambuzi wa Vyeti vya Wanamaji kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya.<br><br>*Agreement between the Government of United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Kenya on Mutual Recognition of Seafarers certificates.* | 04 Mei, 2026 |
| 42. | Hati ya Makubaliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya kuhusiana na Usafirishaji Baharini.<br><br>*Memorandum of Understanding between Tanzania Shipping Agencies Corporation and Kenya Maritime Authority within the Maritime Transport Sector.* | 04 Mei, 2026 |
| 43. | Hati ya Makubaliano kuhusu ushirikiano kati ya Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) na Shirika la Viwango Kenya (KEBS)<br><br>*Memorandum of Understanding between the Kenya Bureau of Standards (KEBS) and Zanzibar Bureau of Standards (ZBS)* | 04 Mei, 2026 |
| 44. | Hati ya Makubaliano baina ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania na Chuo cha Serikali cha Kenya kuhusu | 04 Mei, 2026 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| | kujengeana Uwezo kwenye masuala ya Utumishi wa Umma<br><br>*Memorandum of Understanding between Kenya School of Government and Tanzania Public Service College in the Field of Capacity Development in the Public Service* | |
| 45. | Mkataba wa Kutotoza Kodi marambili na Kuzuia Uepaji na Ukwepaji Kodi kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uturuki<br><br>*The Agreement between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Turkiye for The Elimination of Double Taxation with Respect to Taxes on Income and The Prevention of Tax Evasion and Tax Avoidance (DTA)* | 04 Mei, 2026 |
| 46. | Hati ya Makubaliano kati ya Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Chuo cha MGIMO cha Urusi kuanzisha ushirikiano katika kuendeleza lugha ya Kiswahili<br><br>*Memorandum of Understanding between National Kiswahili Council (Bakita) and Mgimo University establishing Collaboration in the Field of Development of Kiswahili Language.* | 16 Mei, 2026 |

| NA. | JINA LA MKATABA/HATI YA MAKUBALIANO | TAREHE YA SAINI |
|---|---|---|
| 47. | Hati ya Makubaliano kati ya Chuo cha Sayansi Shirikisho cha Muhimbili, na Kampuni ya Raoid Bio ya Urusi na Kampuni ya LifeDX,<br>*Memorandum Of Understanding Between Muhimbili University of Health and Allied Sciences (The United Republic of Tanzania) Rapid Bio LLC (Russian Federation) LifeDX Africa Ltd. (The United Republic of Tanzania).* | 16 Mei, 2026 |
| 48. | Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Rwanda katika Sekta ya Nishati<br>*Memorandum of Understanding between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Rwana on Cooperation in Energy Sector.* | 19 Mei, 2026 |

**Kiambatisho Na. 2: Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki**

1. Ee Mungu twaomba ulinde
Jumuiya Afrika Mashariki
Tuwezeshe kuishi kwa amani
Tutimize na malengo yetu.

***Chorus***

*Jumuiya Yetu sote tuilinde*
*Tuwajibike tuimarike*
*Umoja wetu ni nguzo yetu*
*Idumu Jumuiya yetu.*

2. Uzalendo pia mshikamano
Viwe msingi wa Umoja wetu
Uhuru na Amani
Mila zetu na desturi zetu.

***Chorus***

*Jumuiya Yetu sote tuilinde*
*Tuwajibike tuimarike*
*Umoja wetu ni nguzo yetu*
*Idumu Jumuiya yetu.*

3. Viwandani na hata mashambani
Tufanye kazi sote kwa makini
Tujitoe kwa hali na mali
Tuijenge Jumuiya bora.

***Chorus***

*Jumuiya Yetu sote tuilinde*
*Tuwajibike tuimarike*
*Umoja wetu ni nguzo yetu*
*Idumu Jumuiya yetu.*

**Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

Mji wa Serikali, Mtumba,
**S.L.P 2933,** 40466 DODOMA.

**Mawasiliano:**
**Simu:** +255 26 232 3201-7
**Barua Pepe:** nje@nje.go.tz
**Tovuti:** foreign.go.tz

**mfa_tanzania**